MUHTASARI WA MFUMO WA

# UCHUMI WA SOKO JAMII

KWA TANZANIA

KUELEKEA MAENDELEO SHIRIKISHI
NA ENDELEVU YA KIUCHUMI

ISBN: 978-9987-716-16-6

**Machi 2019**

© Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. (KAS)

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa na kubadilishwa kukidhi mahitaji yanayotakiwa bila kuomba idhini ili mradi mwenye haki miliki ajulishwe na machapisho yote yatolewe bure. Machapisho yoyote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatahitaji kibali kutoka Konrad-Adenauer-Stiftung e. V.

Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. itashukuru kupatiwa nakala ya chapisho lolote ambalo sehemu ya maandishi au vielelezo vyake vimenukuliwa kutoka kwenye kitabu hiki.

Utayarishaji na uchapaji wa chapisho hili umefadhiliwa na Konrad-Adenauer-Stiftung e.V.

Angalizo: Maoni yaliyotolewa na waandishi wa kitabu hiki ni ya kwao wenyewe, wala si msimamo wa KAS.

KONRAD
ADENAUER
STIFTUNG

S.L.P 6992
Mtaa wa Ismani, Upanga
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2153174
www.kas.de/tanzania

# Yaliyomo


**1. Utangulizi** ........................................ **1**

**2. Nadharia ya Uchumi Jamii** ........................................ **2**

2.1. Mifumo ya Kiuchumi ........................................ 2

*2.1.1 Uchumi Unaopangwa na Serikali Kuu* ........................................ 3

*2.1.2 Uchumi wa Soko* ........................................ 3

*2.1.3 Uchumi Jamii* ........................................ 4

2.2 Uchumi Jamii Uliofanikiwa ........................................ 6

*2.2.1 Kanuni za Uchumi Jamii* ........................................ 6

*2.2.2 Wadau* ........................................ 8

**3. Uchambuzi wa Hali ilivyo Nchini Tanzania** ........................................ **9**

3.1 Historia ya maendeleo ya kiuchumi Tanzania ........................................ 9

3.2 Maendeleo ya Uchumi Mkubwa na Mdogo ........................................ 10

*3.2.1 Vigezo Muhimu vya Uchumi Mkubwa* ........................................ 10

*3.2.2 Nyenzo za Uzalishaji* Mali........................................ 13

*3.2.3 Sekta Muhimu* ........................................ 15

3.3 Maendeleo ya Kijamii ........................................ 16

*3.3.1 Umasikini* ........................................ 16

*3.3.2 Hifadhi ya jamii* ........................................ 17

*3.3.3 Afya ya Uzazi na Vifo* ........................................ 17

*3.3.4 Makundi Yaishiyo katika Mazingira Hatarishi* ........................................ 18

3.4 Maendeleo ya Kisiasa ........................................ 20

3.5 Maendeleo ya Kiteknolojia ........................................ 22

3.6 Maendeleo ya Kimazingira ........................................ 23

3.7 Uchambuzi Yakinifu wa Kutambua Uwezo - Udhaifu - Fursa na Changamoto za Tanzania ........................................ 24

**4. Mfumo wa Uchumi Jamii kwa Tanzania** ........................................ **26**

4.1 Mikakati ........................................ 28

4.2 Utekelezaji – Hatua za Utekelezaji ........................................ 43

**5. Hitimisho** ........................................ **47**

# Orodha ya Vielelezo na Majedwali

## Orodha ya Vielelezo


Kielelezo 1: Uchumi Jamii ..................... 5

Kielelezo 2: Historia ya Maendeleo ya Mifumo ya Uchumi Tanzania .. 10

Kielelezo 3: Pato la Taifa na Ukuaji wake Katika Nchi Husika ........... 11

Kielelezo 4: Ajira Nchini Tanzania ..................... 14

Kielelezo 5: Nguzo za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) ................ 22

Kielelezo 6: Vipengele vya Mfumo wa Uchumi ..................... 29

Kielelezo 7: Soko Katika Mfumo wa Uchumi Jamii ..................... 32

Kielelezo 8: Kodi Kulingana na Kipato ..................... 37

Kielelezo 9: Hatua za Utekelezaji ..................... 46


## Orodha ya Majedwali


Jedwali 1: Mlinganisho wa Mifumo ya Uchumi ..................... 4

Jedwali 2: Viashiria vya Uchumi Mkubwa ..................... 10

Jedwali 3: Nyenzo za Uzalishaji Mali ..................... 13

Jedwali 4: Uwezo, Madhaifu, Fursa na Changamoto ..................... 25

# 1. Utangulizi

Nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea zimepitia hatua mbalimbali katika kuboresha maisha ya wananchi wake. Baadhi ya nchi tayari zimefikia malengo yake, nyingine zinahitaji muda zaidi ili ziweze kufikia malengo. Wakati baadhi ya nchi zikiwa na mikakati inayoeleweka, nyingine zimekuwa zikibadili sera zao na kutengeneza mipango mipya. Hata hivyo siyo kila mbinu iliyotumika ilileta matokeo chanya. Hili limekuwa ni tatizo linaloikumba nchi ya Tanzania pia, ambapo mikakati na sera mpya zilizotengenezwa ziliimarisha ukuaji wa uchumi lakini hazikufanikiwa kuwaondoa wananchi kwenye umasikini. Maendeleo ya kweli ya kiuchumi bado hayajafikiwa.

Sababu ya kufanikiwa au kutofanikiwa, inaweza ikawa ni mfumo wa uchumi ambao nchi husika inautumia. Kwa sababu hiyo, ni vema tukaziangalia nchi zinazofanya vizuri kiuchumi na kujifunza kutoka kwao. Mfumo wa uchumi ambao umeleta maendeleo thabiti katika nchi nyingi, mfano Ujerumani na Sweden, unafahamika kama UCHUMI WA SOKO JAMII.

Kitabu hiki kinaelezea kwa muhutsari mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii na kuulinganisha na hali halisi ya sasa nchini Tanzania. Katika hili historia na utamaduni wa nchi utazungumziwa pia. Lengo ni kuonesha njia sahihi kwa maendeleo ya uchumi shirikishi na endelevu kwa Tanzania.

Muhutasari huu kwanza umefanya mapitio ya mifumo ya uchumi duniani na pia kuitambulisha dhana ya Uchumi wa Soko Jamii katika sehemu yake ya pili. Kisha sehemu ya tatu imeangazia hali ya sasa ya uchumi nchini Tanzania na kuchambua maendeleo mbalimbali ambayo nchi imeyafanya. Kutokana na uchambuzi huo, sehemu ya nne (4) inapendekeza mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii ambao utafaa kwa taifa la Tanzania. Sehemu ya tano inatoa hitimisho na kupendekeza namna mfumo huu unavyoweza kuanzishwa na kutumika.

# 2. Nadharia ya Uchumi wa Soko Jamii

Mnamo 2017, Tanzania ilikuwa na idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia 55 milioni. Ni muhimu kwa watu wote hao kuwa na kipato cha kutosha kulisha familia zao, kulipia mahitaji ya kila siku na kuishi maisha yanayostahili. Inakuwa rahisi kushughulikia mahitaji haya muhimu endapo nchi itakuwa imeboresha hali za maisha ya wananchi wake, mfano mishahara mizuri, upatikanaji wa huduma za afya, na elimu bora. Hali ya maisha iliyo bora ni matokeo ya maendeleo. Ili kuhakikisha kwamba jitihada za kazi za Watanzania zinachangia kwenye lengo la maendeleo, usimamizi wa kiuchumi ni muhimu. Hii inamaanisha kwamba kunatakiwa kuwepo muongozo wa kiuchumi ambao utapelekea ukuaji wa uchumi.

Masoko huria yanaweza kusaidia kuimarisha ukuaji wa uchumi kwasababu yanaruhusu watu kufanya kazi kwa ushindani, kuwa wabunifu, na kuanzisha biashara. Kwa minajili hiyo soko huria hukuza uchumi. Hata hivyo, masoko huria yanaweza kuwa hatarishi kwasababu yanawaacha nyuma watu masikini na hayatoi msaada kwa makundi ya kijamii yaliyo pembezoni/yaliyotengwa. Ni muhimu kwa serikali kuzuia hili lisitokee kwa kuweka kanuni bora kwenye uchumi wa nchi. Hili si jambo rahisi. Endepo serikali itaweka udhibiti mkali katika sekta ya uchumi, itawasaidia watu masikini wanaohangaika kutafuta maisha lakini pia itakuwa na matokeo hasi kwenye ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa ujumla. Kazi ya mfumo wa uchumi ni kutafuta usawa kati ya pande hizi mbili za udhibiti wa serikali na masoko huria. Hili linaweza kufanikiwa kwa kutumia mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii.

## 2.1. Mifumo ya Kiuchumi

Hivi karibuni, nchi nyingi zimeboresha mifumo yao ya kiuchumi kwa sababu ni watu wachache tu wamekuwa wakifaidika na ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, sasa hivi lengo ni kuweza kufikia uchumi endelevu na jumuishi ili kuhakikisha kwamba kila mtu ananufaika na ukuaji wa uchumi.

**Jumuishi**

*Jumuishi inamaanisha watu wote wanashiriki katika mipango na malengo mbalimbali, hakuna anayeachwa nyuma. Endapo wazo fulani linahusu watu wote na kuleta manufaa kwa wote, wazo hilo tunasema ni jumuishi.*



**Uendelevu**

*Endelevu inamaaanisha kuwa chochote atendacho mtu leo anatenda kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho. Maamuzi yanayofanyika leo yakiweza kunufaisha kizazi cha sasa na hata cha baadaye, hii inamaanisha uendelevu.*



Nchi nyingi zimejaribu mifumo mbalimbali ya kiuchumi kwa mitizamo tofauti ya namna ya kuleta maendeleo. Miundo ya uchumi inayofahamika zaidi ni miwili, ambayo ni Uchumi wa soko na uchumi unaopangwa na serikali kuu (Uchumi Hodhi). Mfumo wa tatu unaojitokeza ni ule unaofahamika kama mfumo wa uchumi mseto ambao unajumuisha mfumo wa soko huria na ule unaopangwa na serikali kuu.

Mifumo hii inafafanuliwa kama ifuatavyo,

### *2.1.1. Uchumi unaopangwa na serikali kuu*

Katika mfumo huu, uchumi hupangwa na mamlaka moja ambayo ni serikali kuu. Mpango wa kitaifa ndio unaotumika kupangilia shughuli za kiuchumi na kugawanya rasilimali. Ni vigumu kwa mtu mmoja mmoja kufanya maamuzi ya uchumi kwa sababu sehemu kubwa ya uchumi inaendeshwa na serikali kuu. Matokeo yake, sekta binafsi inaweza kudhoofika na kukosa ufanisi.

### *2.1.2. Uchumi wa Soko Huria*

Katika mfumo huu, michakato mbalimbali ya kiuchumi hupangwa na watu binafsi au vikundi. Wafanya biashara hushindana kwa uhuru na kila mmoja anaweza kufanya maamuzi yake katika aina hii ya uchumi. Mahitaji ya soko na kiasi cha bidhaa iliyopo na huduma ndizo zinazopanga bei ya soko. Kutokana na ushindani mkubwa, baadhi ya makundi katika jamii yanaweza kuachwa nyuma.

Mambo ya msingi katika mifumo hii yameainishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 1: Mlinganisho wa Mifumo hii ya Uchumi**

| | **Ujamaa (Uchumi Unaopangwa)** | **Ubepari (Uchumi wa Soko Huria)** |
|---|---|---|
| **Kanuni za Uchumi** | Sera za nchi ndizo zinazoongoza uchumi | Udhibiti unatokana na soko (kanuni ya uchumi ya "supply and demand") |
| **Ardhi, Watu, Mtaji** | Vinamilikiwa na serikali | Vinamilikiwa na watu binafsi/ vikundi (hakimiliki inalindwa) |
| **Haki na Usawa katika Jamii** | **Usawa** Tofauti za kiuchumi na kijamii zinapunguzwa kwa kugawanya rasilimali na mapato ya nchi kwa watu wote. Hii pia inaweza kupunguza ushindani | **Ubinafsi kwa Walionacho** Kiwango kidogo cha mgawanyo wa rasilimali kwenye jamii kwa sababu kinaweza kuathiri soko. Inaaminika kwamba soko ndiyo njia bora kabisa ya kugawanya rasilimali |
| **Kufanya Maamuzi** | **Mamlaka moja kwa Maslahi ya Umma** Mamlaka kuu ya nchi ina udhibiti mkubwa wa michakato ya kiuchumi. Juhudi za mtu mmoja mmoja na hata za sekta binafsi zinabanwa. | **Ugatuzi wa Madaraka** Watu binafsi na sekta binafsi wanaweza kufanya maamuzi yao. |
| **Jukumu la Serikali** | **Udhibiti wa Moja kwa Moja** Serikali inajihusisha moja kwa moja kwenye uchumi kwa kufanya maamuzi kwenye mgawanyo wa rasilimali na mapato. | **Udhibiti Usio wa Moja kwa Moja** Serikali inasaidia masoko kwa kuweka mfumo imara wa kisheria ili kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji na biashara. |

### *2.1.3. Uchumi wa Soko Jamii*


Mfumo wa Uchumi Jamii unajumuisha ukuaji wa uchumi endelevu na ushirikishwaji ili kuleta maendeleo kwa watu wote. Mfumo huu unapendekeza aina ya uchumi wa soko, lakini unahakikisha kuwa

binadamu ndiyo kiini cha shughuli zote za kiuchumi. Kupitia mfumo wa ulinzi na udhibiti katika jamii, binadamu pamoja na ujuzi wao, mahitaji na motisha wanalindwa kikamilifu. Mfumo huu pia unawaheshimu binadamu kama watu huru.

Uchumi wa Soko Jamii unaleta usawa kati ya soko huru na mfumo wa udhibiti wa serikali ulio rafiki kwa biashara. Mfumo huu unaruhusu ushindani wa haki na upangaji wa bei za bidhaa na huduma kwa uhuru. Hii huzalisha ajira, hujenga sekta binafsi zilizo imara na husaidia uchumi kukua.

Mfumo huu ni tofauti na mifumo ya kijamaa inayodhibiti jamii. Mfumo huu pia ni tofauti na mfumo wa kibepari unaoheshimu uhuru wa mtu lakini usio linda jamii zilizo pembezoni/zilizotengwa. Mfumo wa Uchumi Jamii unajumuisha na kuwalinda wazawa katika maendeleo ya kiuchumi katika nchi yao.

**Kielelezo 1: Uchumi wa Soko Jamii**




**UCHUMI WA SOKO JAMII**

Huu ni mfumo maalumu wa uchumi wa soko huria. Unategemea ushindani wa soko ambapo sekta binafsi zinauza na kununua bidhaa kwa uhuru. Bei zinatokana na upatikanaji wa bidhaa na uhitaji wake. Ardhi, rasilimali watu na mitaji inamilikiwa na sekta binafsi na haki milki zinalindwa. Mfumo huu unazingatia sheria, dhima ya uwajibikaji na kanuni imara za kiuchumi. Serikali inarekebisha mfumo wa taasisi ili kuleta ukaribu kwa shughuli za kiuchumi na ustawi wa jamii, usalama wa kijamii na uhuru wa watu binafsi. Unalenga kutoa fursa sawa kwa watu wote na vile vile utajiri mdogo unaoheshimu utu wa mtu.

## 2.2 Uchumi Jamii Uliofanikiwa

Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu kwa mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii uliofanikiwa.

a) **Mifumo thabiti** inayovutia wafanyabiashara kushiriki katika uchumi. Hii inajumuisha sheria, taratibu za nchi na mahakama huru. Pia mfumo huu unatakiwa kunyumbulika vya kutosha ili kuendana na mabadiliko nchini. Hata hivyo bado ni lazima mfumo huu uheshimu matakwa ya watu binafsi na haki za kijamii wakati wote.

b) **Utayari wa serikali kuunga mkono** mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. Serikali ni lazima ihakikishe huduma zinazouwezesha mfumo huu kufanikiwa, kama vile elimu, afya, miundombinu ya mawasiliano na uchukuzi zinapatikana. Hata hivyo, ni lazima iheshimu mipaka yake na kuzipa taasisi nyingine, kama vile benki kuu, nguvu ya kufanya uamuzi.

c) **Vyombo huru vya habari.** Vyombo hivi huwapa taarifa wadau kuhusiana na shughuli za kiuchumi nchini. Taarifa zinaweza kuelezea juu ya bidhaa, sheria na taratibu mpya za nchi, au maendeleo ya kiuchumi. Vyombo vya habari vyenye ufanisi na vya kuaminika vinaweza kusaidia kuimarisha ukuaji wa uchumi.

d) **Uhuru na ushirikiano baina ya wadau** ni wa muhimu ili kufanikisha malengo yao. Washiriki wa uchumi ni lazima wawe huru kuchagua wanachotaka. Hata hivyo, ni lazima wafanye makubaliano na wafanye kazi pamoja kwa sababu wanategemeana.

### *2.2.1. Kanuni za Uchumi wa Soko Jamii*

Uchumi wa Soko Jamii unaongozwa na kanuni kadhaa. Kanuni hizi ni uwezo wa kujitegemea na kujiendesha pamoja na mshikamano.


- **Uwezo wa Kujitegemea na Kujiendesha** ni msingi unaoeleza ni kwa namna gani mtu mmoja mmoja au vikundi vidogo vinaweza kuwajibika kwa mambo yao binafsi. Ngazi ya juu huhusishwa kutoa msaada pale tu ngazi ya chini inapokuwa haiwezi kutatua matatizo yake. Katika mfumo wa kiutawala nchini Tanzania, ngazi za kiutawala ni kijiji, kata, miji, wilaya, halmashauri, manispaa na wizara.

**Mfano: Uwezo wa Kujitegemea na Kujiendesha**

John na Nana ni mapacha. Wanakaribia kuanza mwaka mpya wa masomo na wanahitaji mabegi mapya. Kwa sababu wamekuwa watu wazima, wazazi wao waliwaacha wajichagulie wenyewe rangi na aina ya begi waliyopenda.

Kadiri John na Nana wanavyozidi kukua, inawabidi wafanye uamuzi juu ya shule ya sekondari. Kwa vile hawana taarifa za kutosha kuhusu ubora wa shule na kuhusu kiwango gani cha pesa familia yao inaweza kulipia. Wazazi wa John na Nana wanafanya uamuzi juu ya shule.


Kijiji cha John na Nana hakina barabara kwa hiyo ni vigumu watoto kufika shuleni kwa usalama. Uamuzi kuhusu wapi barabara ijengwe hauwezi kufanywa na John na Nana au wazazi wao kwasababu inawahusu watu wengi. Inawabidi wapeleke mapendekezo ngazi ya juu inayofuata, kwa mfano baraza la kijiji, ambalo ndilo litafanya uamuzi juu ya tatizo hilo.




- **Mshikamano/Umoja** inamaanisha watu kusaidiana. Watu wanapokuwa na mshikamano, husaidiana bila ya kuangalia rangi ya mtu, jinsia, dini au tabia zingine za mtu. Mshikamano pia unahusishwa na kusimamia utu katika uchumi.

**Mfano: Mshikamano hujidhihirisha katika maisha yetu ya kila siku**

- Watoto wakubwa husaidia kuhudumia wadogo zao wazazi wao wanapokuwa kazini.
- Wanafamilia husaidiana pale mmoja wao anapokuwa mgonjwa au anapokwama kiuchumi.
- Wakati mwingine watu huhukumiwa kimakosa, mashahidi husimama imara mahakamani kuhakikisha haki inapatikana



**Kuna misingi mingine muhimu ya Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii**

- Upatikanaji na uhitaji wa bidhaa na huduma hudhibiti bei za bidhaa na huduma katika **soko huria.**
- Wananchi wana haki ya **kumiliki mali** na hii huwapa motisha ya kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi.
- **Serikali na dola husaidia** kuzuia ukiritimba, kusimamia uwajibikaji na kusimamia biashara ya kimataifa ili kusiwe na ukandamizaji kwa wazalishaji wa ndani.
- **Bidhaa za umma na huduma**, kwa mfano elimu, miundombinu na huduma za afya, hutolewa na serikali. Serikali inaanzisha **mfumo wa kodi na hifadhi ya jamii** ili kuwasaidia ambao hawajanufaika na ukuaji wa uchumi.

### *2.2.2 Wadau*

Ili mfumo wa Uchumi Jamii uweze kufanikiwa wadau wake lazima watimize majukumu yao kama ifuatavyo:

- **Serikali kuu na serikali za mitaa**: Hizi huisaidia kuongeza ufanisi wa shughuli mbalimbali kama vile ukusanyaji mapato na kugawa majukumu kwa mamlaka husika. Kutokana na msingi wa *kujitegemea na kujiendesha*, makujumu yanaweza kugawiwa kwa taasisi za ngazi ya chini pale inapowezekana.
- **Mashirika ya umma**: Mashirika haya ni taasisi za kiserikali zinazoshughulikia kazi za kijamii. Mifano ya mashirika haya ni;
  - Mifuko ya hifadhi ya jamii kama vile mafao ya uzeeni, bima ya afya na ajali na fao la kukosa ajira
  - Wawakilishi wa wafanyabiashara,viwanda na kilimo
  - Taasisi za kimataifa kama vile benki za maendeleo
- **Sekta binafsi na serikali** kwa pamoja zinasaidiana kujenga uchumi imara. Lakini umuhimu wa sekta binafsi ni mkubwa kwa kuwa inazalisha ajira nyingi zaidi.
- **Bodi za usimamizi**: Hivi ni vyombo vyenye jukumu la kudhibiti, kusahihisha na kutoa maamuzi ya mambo kwenye maeneo mbalimbali. Bodi hizi ni kama vile benki kuu, taasisi ya usimamizi wa biashara, uzalishaji na madawa. Wadau wengine wanaounda bodi hizi ni vyama vya wafanyakazi na vile vya waajiri.

# 3. Uchambuzi wa Hali ilivyo Nchini Tanzania

Wakati wa kuanzisha mfumo mpya, ni muhimu kufanya uchambuzi wa hali halisi niliyopo ili kugundua changamoto na kuzipatia ufumbuzi kwa namna iliyo bora. Ili kuuelewa mfumo wa uchumi wa soko jamii na namna unavyoweza kutumika Tanzania ni lazima kufanya uchambuzi wa hali halisi ya nchi pamoja na mahitaji ya watu. Maeneo muhimu yanayotakiwa kutazamwa na kufanyiwa uchambuzi ni pamoja na :

a) Maendeleo ya kiuchumi
b) Maendeleo ya kijamii
c) Maendeleo ya kisiasa
d) Maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na
e) Maendeleo ya kimazingira

## 3.1 Historia ya mfumo wa uchumi wa Tanzania

Ili kuweza kuelewa hali ya sasa ya nchi yetu, tutaangalia historia ya mifumo mbalimbali ya kiuchumi iliyowahi kutumika nchini. Mfumo wa uchumi wa Tanzania umebadilika mara nyingi. Mabadiliko haya yanaweza kugawanywa katika vipindi vikuu vitatu.


- **1961-1967: Kutoka Uhuru mpaka Ujamaa**
  Katika miaka ya mwanzoni baada ya uhuru, nchi iliendelea na uchumi wa kibepari wa kikoloni uliotawaliwa na soko huria na kuhodhiwa na matajiri wachache. Kulikuwa na uhuru wa sekta binafsi ingawaje biashara za ndani hazikuendelezwa.

- **Badiliko la mwaka 1967: Ujamaa**
  Azimio la Arusha chini ya utawala wa Mwl Julius Kambarage Nyerere lilibadilisha historia ya Tanzania. Ujamaa wa kiafrika kama ulivyojulikana ukawa ndiyo njia mpya ya kiuchumi na kijamii kwa nchi ya Tanzania. Kipindi chote cha utekelezaji wa Azimio La Arusha, njia zote kuu za kiuchumi zilitaifishwa na mipango yote ya kiuchumi ilipangwa na serikali kutoka makao makuu ya nchi. Biashara zote za serikali zilisimamiwa na mashirika ya umma, ushiriki wa sekta binafsi ulipungua na kiwango cha ukuaji wa uchumi kilishuka.

- **Katikati ya miaka ya 1980-Uchumi wa soko huria**
  Rais Ali Hassan Mwinyi alirudisha mfumo wa soko huria katikati ya miaka ya 1980. Masoko yalifunguliwa, sekta binafsi na uwekezaji vikashamiri. Maboresho zaidi ya kimfumo yalifanyika mwaka 1986 na kuruhusu serikali kutoa baadhi ya huduma za afya na elimu. Hivi sasa Serikali imeanzisha mikakati mipya, kwa mfano, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Tukilinganisha mifumo mbalimbali iliyowahi kutumika kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania, takwimu zinaonesha kuwa mfumo uliooneshа matokeo bora zaidi ni wa soko huria. Hata hivyo matokeo yaliyokusudiwa ya kuwaletea wananchi unafuu wa maisha bado hayajafikiwa kikamilifu.

**Kielelezo 2: Historia ya Maendeleo ya mifumo ya uchumi Tanzania**




## 3.2 Maendeleo ya uchumi mkubwa na mdogo

### *3.2.1 Vigezo muhimu vya uchumi mkubwa*

Ukuaji endelevu wa uchumi unawezekana tu endapo mfumo wa uchumi mkubwa utakuwa imara. Uchumi mkubwa huhusisha viashiria vya jumla na maendeleo ya uchumi. Wakati viashiria hivi vikiwa na maendeleo chanya, ukuaji wa uchumi unaweza kutokea. Baadhi ya viashiria muhimu vya uchumi mkubwa vimeorodheshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2: Viashiria vya Uchumi Mkubwa**

| Viashiria vya Uchumi Mkubwa | Tafsiri |
|---|---|
| Pato Ghafi la Taifa (GDP) | Pato ghafi la taifa (GDP) ni thamani ya jumla ya bidhaa zilizotayari kuuzwa pamoja na huduma zilizozalishwa ndani ya mwaka mmoja. Hiki ni kipimo cha fedha kinachoonyesha uimara na ukubwa wa uchumi wa nchi husika. |
| Kiwango cha Mfumuko wa Bei | Kiashiria hiki hupima ongezeka la bei kwa bidhaa na huduma ndani ya muda Fulani. Ni kawaida kupima kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwaka. Kiwango cha mfumuko kinatakiwa kuwa chini na tulivu. |


| | |
|---|---|
| Viwango vya Riba | Hiki ni kiasi cha pesa (hujulikana kama riba) ambacho hutozwa kutokana na mkopo wa fedha. Riba ni kwa asilimia ya kiasi cha jumla kilichokopwa. |
| Bei za Bidhaa | Hii inazungumzia bei za bidhaa za msingi ambazo huweza kuuzwa sokoni. Bei hizi ni za bidhaa na huduma zilizoko sokoni |
| Thamani ya Sarafu | Thamani ya sarafu ya nchi hutegemea uhitaji wake sokoni. Thamani ya sarafu ndiyo hupima uhitaji wake na kuuelezea kwa mlinganisho na sarafu zenye thamani kubwa zaidi, mara nyingi huwa ni dola ya kimarekani. Kiwango cha kubadili fedha hupangwa kutokana na sarafu zenye thamani kubwa. |
| Uwiano kati ya mauzo nje ya nchi na kuagiza bidhaa kutoka nje | Kiashiria hiki huangalia uchumi wa nchi kama akaunti ya benki. Kiashiria hiki kinapima mapato yote na matumizi ya nchi. Uwiano huu unaweza kuwa ziada (mapato yanapozidi matumizi) au nakisi (matumizi yanapozidi mapato). |

## Pato Ghafi la Taifa (GDP)

Nchini Tanzania, pato la taifa limekuwa likikua kwa kiwango cha kuridhisha tangu miaka ya 1990. Kiwango cha ukuaji kimekuwa ni kwa wastani wa asilimia 6.5, ambacho ni miongoni mwa viwango vya juu kabisa vya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki. Jedwali lifuatalo linaonesha kuwa ingawa Tanzania ina kiwango kikubwa cha ukuaji wa pato la taifa miongoni mwa nchi zilizoorodheshwa, bado Tanzania ndiyo nchi yenye pato la jumla la chini zaidi kuliko nchi nyingine.

> Pato la taifa ni jumla ya matumizi ya kibinafsi, uwekezaji wa biashara, matumizi ya serikali na tofauti kati ya mauzo ya nje na mapato yatokanayo na kuagiza biadhaa kutoka nje.

**Kielelezo 3: Pato ghafi la taifa na ukuaji wake katika nchi husika**



**Hadhi ya Uchumi wa Kipato cha Kati**

Lengo kuu mojawapo katika ajenda ya Tanzania ya viwanda ni kufikia hadhi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Hii ina maana ya kuwa na wastani wa pato la mwezi la dola za Kimarekani 1006-12,235 kwa mtu mmoja. Mwaka 2017, Tanzania haikufikia lengo la uchumi wa kati ikiwa na pato la taifa la dola 910 kwa mtu mmoja mmoja, na kuangukia kwenye kundi la nchi masikini/zenye uchumi wa chini. Nchi nyingine 33, kama vile Uganda, Rwanda, Burundi, sudani kusini, Malawi na Msumbiji nazo zinaangukia kwenye kundi hili.

**Mfumuko wa bei, viwango vya riba na thamani ya shilingi**

Kiwango cha mfumuko wa bei kinaonesha mwelekeo mzuri. Mfumuko wa bei umekuwa tulivu na umeshuka kidogo kufikia kiasi cha 5.2% kwa mwaka 2016. Viwango vya riba pia vimebakia kwenye hali yake ya kawaida ya asilimia 14 mpaka 16. Vile vile thamani ya shilingi ya Tanzania imebakia kuwa tulivu. Hapo mwaka 2015, dola 1 ya kimarekani ilibadilishwa kwa shilingi za kitanzania 1,985. Kufikia oktoba 2018, kiwango cha ubadilishaji wa fedha kilipanda hadi kufikia shilingi za kitanzania 2,278 kwa dola 1 ya kimarekani.

**Bei za bidhaa na uwiano wa mauzo ya ndani na ya nje**

Uchumi wa Tanzania umekuwa tegemezi sana kwa bei za bidhaa za nje. Kwa miaka iliyopita, bei za bidhaa nyingi zimeshuka kutokana na kubadilika kwa mahitaji ulimwenguni. Bei za mafuta, dhahabu na chuma ziliathiriwa kwa kiasi kikubwa kwa vile mauzo ya bidhaa nje ya Tanzania yanahusisha bidhaa za aina chache na kwa kiasi kikubwa ni bidhaa ghafi. Mabadiliko ya bei katika soko la dunia yanaathiri moja kwa moja mauzo nje ya nchi. Hii inamaanisha kuwa thamani ya soko la nje ikiporomoka ni tatizo kubwa kwa uchumi wa Tanzania. Hata hivyo kwa ujumla Tanzania ni miongoni mwa nchi chache za Afrika ya Mashariki ambazo bado zina kiwango cha chini cha mauzo ya nje.

**Mageuzi ya uchumi na viwanda**

Miongoni mwa mabadiliko muhimu kiuchumi ni pamoja na ubinafsishwaji wa viwanda vya umma na maboresho ya miundombinu ya nchi, miundombinu ya mitandao ya simu, na upatikanaji wa huduma za mtandao. Hivi karibuni, sekta zinazokua kwa kasi kubwa, zimekuwa ni sekta za habari na mawasiliano, fedha na bima, ujenzi, biashara ya jumla na reja reja na sekta ya uzalishaji viwandani.

Wakati Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano ukisisitiza ukuaji endelevu na maendeleo ya viwanda, sekta ya uzalishaji mali ambayo ndiyo inatakiwa kuongoza maendeleo haya inakumbana na changamoto nyingi. Sekta inakumbana na vikwazo vya kitekinolojia, fedha, vikwazo vinavyotokana na sera na utawala na imeshindwa kuwa na mwendelezo mzuri wa ukuaji. Viwanda katika sekta hii vinapungukiwa mnyororo wa thamani na hivyo kuathiriwa na hali ya soko na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Sekta binafsi za wazawa hazijanufaika na ukuaji wa uchumi ukilinganisha na makampuni makubwa ya nje yaliyowekeza nchini. Kwa vile makampuni ya wazawa hayawezi kushindana kitaifa na hata kimataifa, yamekuwa na wakati mgumu kukua. Ukosefu wa uwekezaji na ubadilishanaji hafifu wa teknolojia, umesababisha mabadiliko yoyote ya kiuchumi yanayofanyika kuwa na kasi ndogo. Hapajawa na mfumo jumuishi wa uchumi unao unganisha mchango wa sekta binafsi na maisha ya wazawa au unaozalisha ajira na kuboresha huduma za afya na elimu.

### *3.2.2 Nyenzo za uzalishaji mali*

Kuna mambo makuu matatu ya msingi katika uzalishaji mali, nayo ni watu, ardhi na mtaji. Jedwali lifuatalo linaelezea sifa zake.

**Jedwali 3: Nyenzo za Uzalishaji Mali**


| Nyenzo za uzalishaji mali | | Sifa |
|---|---|---|
| **Watu/nguvu kazi** |  | Kila aina ya kazi ya mwanadamu hufanywa kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya wengine na kwa wakati huo huo kujipatia kipato binafsi. |
| **Ardhi** |  | Ni chanzo asilia cha rasilimali zote za dunia. Inajumuisha ardhi ambapo juu yake hujengwa viwanda vyote, na ardhi ya kilimo na misitu, madini ya aina zote, maji ya bahari, maziwa na mito na uoto wa asili. |
| **Mtaji** |  | Bidhaa zote ambazo zimetengenezwa lakini bado hazijatumika, lakini zinaweza kutumika kuzalishia bidhaa zingine. Inajumuisha mfano majengo ya viwanda, mashine, nyenzo, bidhaa zilizotengenezwa tayari ambazo bado hazijauzwa. |

Ubora na idadi ya **nguvu kazi/rasilimali watu** ina uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa uchumi. Kwa hivyo ujuzi, uwezo wa ubunifu, mafunzo na elimu ni mambo ya muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Mwaka 2012, idadi ya watu nchini Tanzania ilifikia 44.9 milioni. Kiasi kinachokaribia nusu ya idadi hiyo ilikuwa ni wenye umri wa kati ya miaka 15 na 64, ambao wanahesabika kuwa ni watu walio katika umri wa kufanya kazi. 13% ya idadi hiyo hawakuwa wakishiriki kwenye shughuli za kiuchumi kwa sababu ni wanafunzi au wamestaafu. Katika idadi iliyobakia ya watu 22.45 milioni, watu 20.13 milioni walifanya kazi kwenye sekta rasmi au zile ambazo sio rasmi. Hii ni kumaanisha kwamba kiasi kinachokaribia watu 2.31 milioni ya wale walio katika umri wa kufanya kazi hawakuwa na kazi. Ukosefu wa ajira ulikuwa mkubwa zaidi vijijini.

Idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi inazidi kuongezeka, na inakadiriwa kuwa karibu watu milioni 1 wanaingia katika kundi hili la umri wa kufanya kazi kila mwaka. Hata hivyo soko la ajira linaweza kuzalisha ajira 60,000 tu kwa mwaka katika sekta zilizo rasmi. Hii ina maana kwamba kila mwaka karibu Watanzania 940,000 wanaoingia katika soko la ajira wanakuwa aidha hawana ajira au wanafanya kazi katika sekta isiyo rasmi/ uchumi usio rasmi. Hata hivyo utoaji wa ajira mpya kwa wafanyakazi wapya imekuwa ni tatizo kubwa.

**Kielelezo 4: Ajira nchini Tanzania**



Rasilimali **ardhi** pia inakabiliwa na changamoto kadhaa kwa sasa. Tanzania ina bahati ya kuwa na sehemu kubwa ya nchi kavu yenye rutuba na madini na urefu wa pwani ya bahari, mito, maziwa, kwa mfano ziwa Victoria na bahari ya Hindi. Kwa ujumla fursa hizi za uwepo wa rasilimali nyingi nchini hazitumiwi vizuri, kwa mfano matumizi ya hovyo ya ardhi na kuingiliwa kwa ardhi ya kilimo na hifadhi za misitu. Mazingira hayatunzwi au kutumiwa ipasavyo. Kuna umuhimu mkubwa kuliongelea suala hili kwasababu asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea mazingira yanayowazunguka kujitengenezea kipato.

### *3.2.3 Sekta Muhimu*

Hizi ni sekta zinazoendesha uchumi wa Tanzania. Ni sekta zenye uhusiano wa kipekee kwa sababu zinaajiri idadi kubwa ya watu au zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi. Sekta hizi zimeainishwa hapa chini.

| | |
|---|---|
|  | Sekta ya kilimo ni muhimu kwa sababu ndio mwajiri mkuu wa watu, karibu theluthi mbili (2/3) ya Watanzania. Kwa vile sekta hii inahusisha zaidi kilimo cha kujikimu, inachangia kwa kiasi kidogo sana cha theluthi moja (1/3) tu kwenye pato la taifa. Sio kilimo cha kisasa, hivyo hutegemea zaidi mvua za msimu. |
|  | Sekta ya nishati ina umuhimu mkubwa sana katika mchakato wa kuelekea kwenye uchumi wa viwanda. Tanzania inatumia zaidi nishati itokanayo na nguvu ya maji ambayo ina changamoto kubwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Nishati zitokanazo na jua, upepo na makaa ya mawe zinaongezeka lakini bado hazijaweza kuendelezwa na kutumiwa vya kutosha .Watanzania walio wengi bado hawajaunganishiwa umeme wao wa majumbani kwenye gridi ya taifa. Inakadiriwa 90% ya wananchi wote, wanajitengenezea nishati yao wenyewe inayotokana na maliasili ya miti na misitu hasa kuni na mkaa ambayo ina athari kwa mazingira. |
|  | Sekta hii ya usafirishaji imeendelea kwa kiasi kikubwa. Ujenzi wa barabara za lami umeboresha na kusaidia kuunganisha makao makuu yote ya mikoa nchini. Vile vile ujenzi wa reli mpya ya kisasa umeanza. Reli hii itasaidia kuunganisha Dar es salaam na ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, Burundi , Rwanda , Uganda na jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Usafiri wa anga na majini bado unakumbana na changamoto kwa sababu nyenzo zinazotumika na huduma zitolewazo hazijafikia viwango stahiki. |

| | |
|---|---|
| | Sekta ya mawasiliano imepiga hatua kubwa. Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye gharama ndogo kabisa za vifurushi vya intaneti barani Afrika na mkongo wa mawasiliano umekamilika kwa kutandaza nyaya nchi nzima kuunganisha mikoa yote ya Tanzania bara ambayo ndio msingi wa kuunganisha watumiaji wote. |
| | Mtaji na masoko bado vinahitaji kuboreshwa. Imekuwa vigumu kwa Watanzania kupata mitaji kwa sababu walio wengi hawajui ni vipi wataipata au ni wapi wataiwekeza. Mabenki na taasisi zinazotoa huduma za kifedha zimeongezeka na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha. Hususani kuenea kwa huduma za kifedha zitokanazo na mitandao ya simu za mkononi zimesaidia kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, kwa Watanzania walio wengi, upatikanaji wa mikopo na mitaji bado ni tatizo kubwa kwa sababu hawana utaratibu wa kuweka akiba. Nchini Tanzania, mazingira ya biashara yameonesha mwelekeo chanya na vile vile mwelekeo hasi. Upatikanaji wa mikopo na huduma ya umeme uko katika kiwango cha wastani ukilinganisha na nchi zingine duniani. Hata hivyo biashara ya nje ya mipaka na urahisi wa kuanzisha biashara nchini uko chini kulingana na vigezo vya benki ya dunia. Kumekuwa pia na malalamiko kuhusu ugumu wa kusajili mali na kuongezeka kwa ada za usajili wa ardhi na mali. |

Kwa ujumla, matatizo yatokanayo na sera, ugawaji wa nishati, upatikanaji wa ardhi na ukosefu wa wataalamu wenye vigezo unafanya mchakato wa maendeleo ya viwanda na maendeleo ya Tanzania kwa ujumla kuwa mgumu.

## 3.3 Maendeleo ya Kijamii

### *3.3.1 Umasikini*

Kuna nadharia mbalimbali zinazotumika kupima umasikini, baadhi ya nadharia zinatumia viashiria vya kifedha wakati nadharia zingine zinahusisha upatikanaji wa huduma kama elimu na afya. Kwa mfano mstari wa chini wa umasikini, hupima kiwango cha umasikini kwa watu walio na kipato cha chini ya dola 1.9 kwa siku. Mahitaji ya msingi yanayoangaliwa na mstari wa chini wa umasikini ni upatikanaji wa chakula, maji na malazi. Nchini Tanzania, Umasikini wa mahitaji muhimu umepungua kwani huduma za afya, elimu na upatikanaji wa maji na chakula umeboreka.

Pamoja na kwamba inasemekana umasikini nchini umepungua, kiuhalisia bado wananchi wengi ni masikini kwa sababu ongezeko la idadi ya watu bado ni kubwa mno. Maendeleo ya watu ni ya kiwago cha chini na inakadiriwa Watanzania 12 milioni bado wanaishi kwenye umasikini uliotopea. Hii inaonesha kuwa ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa umewanufaisha watu wachache na sio sekta binafsi ya wazawa.

### *3.3.2 Hifadhi ya Jamii*

Mifumo ya hifadhi ya jamii inatoa msaada wa uangalizi wa afya na msaada wa kifedha ili kutokomeza umasikini. Kwa kawaida mifuko hii hutoa mafao ya ugonjwa, ulemavu, huduma za kujifungua na mafao ya uzeeni. Nchini Tanzania, chini ya 10% ya Watanzania wote ndio wanaoweza kujiunga na mifuko hii kwa sababu ndio walio katika mfumo rasmi wa ajira, yaani ajira za mkataba pamoja na waajiri waliosajiliwa. Watanzania walio wengi hutegemea familia zao au jamii katika kusaidiana.

Hivi karibuni, watu waliojiajiri na wafanyakazi wa sekta zisizo rasmi wamepata nafasi ya kujiunga kwa hiari kwenye mifuko hii ya hifadhi ya jamii na hulipia michango yao ya kila mwezi. Hata hivyo wananchi wengi hawajawa na ufahamu wa kutosha kuhusu mifuko hii, namna ya kujiunga lakini pia kuhusu umuhimu wa mifuko hii.

Vilevile mifuko ya kijamii imeruhusiwa kutumia michango ya wanachama wake na kuwekeza katika maeneo mbalimbali ili kukuza mtaji. Hata hivyo, pesa zingine zimekuwa zikiwekezwa kwenye miradi hatarishi sana na kumekuwa na malalamiko juu ya matumizi mabovu ya michango ya wanachama.

### *3.3.3 Afya ya Uzazi na Vifo*



Kuongezeka kwa uzazi, kupungua kwa vifo vya watoto wachanga na watoto na kuongezeka kwa umri wa kuishi ni sababu za msingi za kuongezeka kwa idadi ya watu nchini. Kwa wastani kila mwanamke wa kitanzania ana uwezo wa kuzaa watoto 5.5 katika maisha yake. Hata hivyo huu ni wastani wa jumla kwani kwa upande wa vijijini hali ni tofauti kidogo. Wanawake wa vijijini wanazaa sana kuliko wale wa mjini. Hapo mwaka 2012 vifo vya watoto wachanga vilipungua na kufikia vifo 68 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai. Kuongezeka kwa idadi ya watu kumekuwa

kukionekana zaidi kutokana na kuongezeka kwa umri wa kuishi. Ambapo mtoto aliyezaliwa mwaka 2002 angetarajiwa kuishi hadi miaka 51,umri wa kuishi kwa watoto waliozaliwa 2012 ulikuwa ni miaka 61. Maambukizi ya VVU/ UKIMWI, TB na malaria yamepungua kwa kiasi kikubwa. Idadi ya Vifo vitokanavyo na upungufu wa kinga mwilini imeshuka kidogo, maambukizi ya malaria pia yanaonekana dhahiri kushuka hasa kwa watoto. Pamoja na mwenendo huu chanya, bado vifo vya watoto wachanga wanaozaliwa vimebakia juu. Utapiamlo na lishe duni vimeendelea kuwa tishio kwa maendeleo ya binadamu nchini.

Sekta ya afya imekuwa na uhaba wa wataalamu na vitendea kazi hususani kwa maeneo ya vijijini Watanzania walio wengi hawawezi kufika kwenye vituo vya afya kwa sababu ya ubovu wa miundombinu, mifumo mibovu ya utoaji wa huduma za afya na umasikini.

Ni wananchi wachache wenye bima ya afya au wanaoweza kulipia huduma za afya. Nchini kote, mfuko wa taifa wa bima ya afya kwa kiasi kikubwa unahudumia sekta rasmi lakini pia unatoa bima ya afya ya hiari kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi wanaoweza kulipia michango yao. Mfuko unaofahamika kwa jina la bima ya afya ya jamii ulianzishwa ili kuwasaidia watu wa vijijini kuweza kupata huduma za afya kwa gharama nafuu. Mifuko hii imeongeza idadi ya wanachama lakini bado kasi yake ya kuwafikia watu wengi zaidi ni ndogo.

Matumizi na usafirishaji wa madawa ya kulevya ni tatizo jingine linalosumbua afya za wananchi. Nchi ya Tanzania imekuwa ndiyo njia ya kupitishia madawa ya kulevya. Bangi inalimwa kwa matumizi ya ndani na hata kwa kuuza nje. Kumekuwa na taarifa za matumizi ya kokeini, hiroini na bangi na hata mirungi. Serikali imejaribu kufanya kampeni mbalimbali za kupambana na matumizi ya madawa ya kulevya na imeweza kuwakamata wauzaji wakuu wa madawa hayo.

### *3.3.4 Makundi yaishiyo katika mazingira hatarishi*

Makundi haya ni kama vile wanawake, wasichana, watoto, wazee na walemavu wa aina zote. Endapo tahadhari maalumu haijachukuliwa ni rahisi kwa makundi haya kusahaulika katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi. Uchumi Jamii unajumuisha kila mwananchi bila kubagua kundi lolote ili kuleta maendeleo ya kiuchumi yanayotarajiwa kwa watu wote.

- **Familia Zinazoongozwa na Wanawake**: Mwaka 2012, asilimia 58 ya wanawake walikuwa wameolewa. Karibia theluthi moja ya familia zote nchini zinaongozwa na wanawake. Idadi hiyo ilikuwa kubwa kidogo kwa mijini kuliko vijijini. Wanawake wanakumbana na vikwazo vingi vya kijamii na kiuchumi vinavyohusu usawa wa kijinsia.
- **Familia za Mzazi Mmoja**: Familia hizi ziko kwenye hatari kubwa ya umasikini kwa sababu shughuli mbalimbali za familia zinafanywa na mtu mmoja. Ni kazi ngumu kwa mzazi mmoja kulea familia, kulipia chakula, malazi, elimu na afya kwa wakati mmoja.
- **Wazee (zaidi ya miaka 60):** Kundi hili linakaribia 6% ya Watanzania wote. Mara nyingi wazee walio katika umri huu hawawezi tena kufanya kazi na kujitengenezea kipato. Wazee ambao ndiyo walezi wa watoto wadogo wako kwenye hatari zaidi ya umasikini. Wanawake waliozeeka nao wako kwenye mazingira hatarishi kwa sababu wanatuhumiwa kwa uchawi na wakati mwingine wanavamiwa na kuuawa.
- **Watoto**: Watoto wanategemea watu wakubwa kuwalinda na uonevu na umasikini. Watoto hawawezi kujisimamia wenyewe, hivyo wanahitaji msaada. Familia zenye watoto wengi ziko kwenye hatari zaidi ya kutumbukia kwenye umasikini uliokithiri. Kwa hiyo watoto wengi hulazimishwa kuacha shule na kurudi nyumbani kuwasaidia wazazi wao kutengeneza kipato. Hii sio sahihi kisheria kwa sababu watoto wana haki ya kupata elimu na kulindwa kutokana na ajira za utotoni. Wasichana wadogo wako kwenye hatari nyingine ya mimba za utotoni zinazowazuia kuhudhuria shule.
- **Jamii za Pembezoni au Zilizotengwa**: Nchini Tanzania baadhi ya jamii zimetengwa kwa sababu ya mahali zilipo na miundombinu iliyopo. Jamii mbalimbali za wawindaji, wakusanyaji bidhaa za chakula, wachungaji, wahamiaji na wale wasiojishughulisha na chochote cha maana wanakumbana na matatizo mengi kwa sababu mtindo wa maisha wanayoishi umefanya kuwa vigumu kwa serikali kuchukua taarifa zao na kutatua changamoto walizonazo. Jamii hizi mara nyingi hazipati huduma za afya, maji na elimu. Lakini baadhi ya jamii hizi zimeanza kukodi ardhi na kuanzisha makazi ya kudumu na wameweza kujichanganya na jamii nyingine na kubadilishana uzoefu.
- **Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi (Albino):** Watu wenye ulemavu wa ngozi mara nyingi hutengwa katika jamii kwa sababu ya ubaguzi,

migogoro na hata kutishiwa kuuawa. Programu mbalimbali za serikali, taasisi zisizo za kiserikali pamoja na makundi ya kijamii zimeshindwa kutokomeza unyanyapaa huu pamoja na imani na tamaduni zinazowabagua watu hawa kwenye jamii.

## 3.4 Maendeleo ya Kisiasa

Tangu uhuru, kumekuwa na juhudi mbalimbali zinazolenga kufikia maisha bora na kuleta maendeleo jumuishi kwa wananchi. Mbinu mbalimbali za kisiasa zimekuwa zikibadilika na zimekuwa na matokeo makubwa katika ukauaji wa uchumi.

Katika maendeleo ya mfumo wa kisiasa nchini Tanzania, mfumo wa vyama vingi ulirudishwa tena mnamo mwaka 1992. Chama cha mapinduzi (CCM) kimeendelea kushika madaraka, lakini pia vyama vingine vya upinzani vimeanzishwa, mfano Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Wananchi (CUF) na vyama vingine 16.

Sera mbalimbali zimetungwa nchini Tanzania hasa upande wa elimu, soko la jira, ajira na uhusiano kati ya nchi na nchi na zinatarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni.

> **Mfumo wa vyama vingi** ni mfumo wa kisiasa ambapo vyama mbalimbali vinakuwa na haki ya kufanya kazi na kushiriki katika uchaguzi wa viongozi. Mfumo huu hupanua demokrasia na kuimarisha utawala bora. Chama tawala huunda serikali wakati vyama vya upinzani vitapima na kukosoa utendaji wa serikali.

### Sera ya Elimu



Serikali ya Tanzania imefanya kazi kubwa kuhakikisha elimu inapatikana kwa urahisi. Tangu Januari 2016, kila mtoto mwenye umri wa kusoma anaweza kupata **elimu ya msingi bure**. Ada kwa shule za msingi na sekondari zimeondolewa na nchi imepiga hatua muhimu katika kufanikisha lengo la nne la maendeleo endelevu la **elimu bora na yenye manufaa**.

Mabadiliko ya mfumo wa elimu yameleta changamoto mpya. Tangu mamia ya wanafunzi wasajiliwe mashuleni kwa mara ya kwanza, kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa waalimu. Lakini pia hakuna vitendea kazi vya kutosha, madawati, vitabu n.k. Kuna haja pia ya kuwasaidia wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwapatia mahitaji ya shule kama madaftari, penseli na chakula wanapokuwa mashuleni.

Mtaala wa elimu wa Tanzania umekuwa ukibadilishwa mara kwa mara na hivyo kuwachanganya walimu na watunzi wa vitabu kutokana na maudhui yake na hivyo kusababisha uchapishaji wa vitabu vipya vyenye makosa mengi. Kwa kiasi kikubwa mabadiliko haya yamekuwa yakifanywa kawa sababu za kisiasa na hayajaleta maboresho ya kweli ya maudhui ya mitaala.

Haijawa wazi ni kwa namna ipi lengo la elimu bora litafikiwa. Mfumo wa elimu uliopo hauendani na mahitaji ya soko la ajira, uchumi, jamii n.k. Elimu yetu haitoi fursa ya kuwapa wanafunzi mbinu za msingi au ujuzi wa kiufundi utakaowawezesha kuanzisha biashara au kutafuta ajira. Kupata elimu ya chuo imekuwa ni vigumu. Hata hivyo kutokana na ufundishaji, mitaala na vitendea kazi duni elimu ya Tanzania imekuwa ikizalisha wahitimu wasio na vigezo na wasioweza kushindana katika soko la ajira. Uhusiano kati ya sera ya elimu na mpango wa maendeleo wa taifa na mahitaji halisi ya soko la ajira bado si mzuri sana. Tunahitaji falsafa ya elimu yenye kujitosheleza ili kunusuru hali hii.

**Nguvu Kazi na Sera ya Ajira**

Sera ya taifa ya ajira ya Tanzania inajaribu kupunguza ukosefu wa ajira. Kwa sasa tatizo la ajira hasa kwa vijana bado ni kubwa. Wengi miongoni mwao wanafanya kazi za uchuuzi na wanakumbana na changamoto nyingi katika kundeleza maisha yao. Tanzania inahitaji mfumo mpya wa kiuchumi ili kuzalisha ajira zaidi na kuhakikisha kwamba vijana wana ujuzi utakaowawezesha kuajiriwa na kujiajiri. Lakini pia mazingira ya upatikanaji wa ajira yanatakiwa kuboreshwa.


**Sera ya Ushirikiano wa Kimataifa**

Tanzania inalenga kukuza uchumi wa kiushindani, kuvutia wawekezaji na kutangaza biashara zake. Hii itasaidia kuingia kwenye masoko ya kimataifa kwa kujiamini. Tanzania imejiunga na mashirika mbalimbali ya kikanda ya biashara, kwa mfano, mpango wa sheria maalumu ijulikanayo kama African Growth Opportunity Act (AGOA) na shirikisho huru la kibiashara

yaani Continental Free Trade Area (CFTA) yanayolenga kurahisisha ufanyaji wa biashara za kimataifa.

Tanzania pia ni sehemu ya jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Jumuiya hii inaundwa na nchi za Burundi, Kenya, Rwanda, sudani ya kusini, Uganda na Tanzania. Jumuiya ya Afrika Mashariki ina watu wapatao 150 milioni. Jumuiya hii ni muhimu sana kwa soko la bidhaa za Tanzania lakini inakumbana na ugumu kwani ushirikiano huu wa jumuiya ya Afrika Mashariki unasuasua hasa kwenye soko na sarafu ya pamoja.

**Kielelezo 5: Nguzo za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC)**




## 3.5 Maendeleo ya Kiteknolojia

Kinadharia, ukuaji wa uchumi unasaidiwa sana na maendeleo ya teknolojia na matumizi ya mbinu na njia za kisayansi. Nchi inapouwekezaji vya kutosha kwenye maendeleo ya kiteknolojia, inaweza kuendelea kwa kasi kwa sababu matumizi ya teknolojia sahihi yanasaidia kuongeza uzalishaji katika taifa hata kama rasilimali ni chache.

Tanzania hutumia 1% ya pato lake la taifa kwa shughuli zinazohusu sayansi, teknolojia na uvumbuzi. Matokeo ya uwekezaji huu ni madogo kwa sababu serikali haiwekezi vya kutosha kwenye kufanya utafiti. Kwa vile kuna uwekezaji mdogo kwenye sekta hii, kumekuwa pia na mchango mdogo wa kifedha kutoka kwenye sekta binafsi kwa ajili ya kuwekeza.

Hali ya utafiti nchini bado iko nyuma na hivyo matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanywa hayawezi kukusanywa na hivyo hayawezi kutumika kwa maendeleo ya viwanda. Ukilinganisha na nchi zingine, Tanzania inashika nafasi ya chini kwenye matumizi ya teknolojia na kuingia kwenye mfumo wa kidijitali ukiilinganisha na nchi kama Uganda,Kenya na Nigeria.

Kwa ujumla, hakuna matumizi ya kutosha ya teknolojia mpya na za kisasa kutokana na gharama kubwa za uendeshaji. Lakini pia hakuna uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa kutumia teknolojia hizi. Endapo Tanzania inataka kufanikiwa kwenye mpango wake wa uchumi wa viwanda, inahitaji kubadili mtizamo wake na kuwekeza katika teknolojia.

## 3.6 Maendeleo ya Kimazingira

Maliasili za nchi zinajumuisha mimea, viumbe vya majini na muonekano wa nchi ulivyo, pamoja na mafuta, gesi asilia, chuma na madini mengine. Maliasili za nchi yoyote zinategemea tabia nchi na mazingira yake yalivyo na matumizi ya maliasili hizo hutegemea ujuzi na uwezo wa nguvu kazi iliyopo, teknolojia inayotumika udhibiti wa serikali iliyopo, upatikanaji wa mitaji na mgawanyo wa mapato. Maliasili zote ni lazima zitumike kwa namna endelevu na kunufaisha vizazi vyote vilivyopo na vijavyo.

Tanzania ni nchi iliyojaliwa sana neema ya kuwa na maliasili nyingi na matumizi yake endelevu yanaweza kuwa ni ufunguo wa uhakika wa mabadiliko ya kiuchumi. Kwa mfano nchi ina utajiri mkubwa wa wanyamapori wa aina nyingi, misitu ya asili, fukwe nzuri na safi, milima, mito, maziwa, madini na gesi na tabia nchi nzuri ya kitropiki na utamaduni mzuri unaovutia watalii kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Tanzania ina utajiri mkubwa wa rasilimali endelevu. Rasilimali hizo ni pamoja na maji, makaa ya mawe, upepo, jua na mabaki ya takataka za mimea. Kati ya hizi maji ni chanzo kikubwa cha uzalishaji wa umeme. Hata hivyo, mabadiliko ya hali ya hewa na matatizo katika mifumo ya usambazaji

imepelekea kuwa vigumu kutegemea nishati ya umeme itokanayo na nguvu ya maji pekee. Tanzania ingeweza kutumia njia mbadala za kuzalisha nishati ya umeme ambazo zina uwezo mkubwa wa kuzalisha nishati hiyo, mfano, umeme utokanao na makaa ya mawe, upepo, nishati ya jua pamoja na mabaki ya takataka za mimea.

Kwa sasa, nchini Tanzania, 90% ya vyanzo vya nishati zitumikazo majumbani zinatokana na sekta ya misitu (mfano, kuni na mkaa). Inakadiriwa kuwa Watanzania milioni 1 wanajihusisha na biashara ya mkaa. Sekta ya misitu pia inachangia kwa takribani nusu ya vifaa vya ujenzi nchini, hivyo umuhimu wake ni mkubwa.

Mpaka sasa, maliasili zilizopo hazitumiwi ipasavyo. Ongezeko kubwa la idadi ya watu na kiwango kikubwa cha umasikini vimechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza tatizo hili. Misitu inakatwa na kutumika kwa kasi ya juu, bayoanuai inapotea na vyanzo vya maji vinaharibiwa. Matokeo yake ni rasilimali kupungua na hivyo kusababisha baa la njaa na umasikini. Kwa vile idadi kubwa ya watu wanategemea zaidi sekta ya kilimo, hii inaongeza msukumo zaidi wa kuanza kutumia sera za kimazingira ili kuwepo na matumizi endelevu ya rasilimali zetu.

## 3.7 Uchambuzi Yakinifu wa Kutambua Uwezo - Udhaifu - Fursa na Changamoto za Tanzania

Matokeo ya uchambuzi wa hali ya kiuchumi na kijamii ilivyo nchini umefafanuliwa kwenye jedwali lifuatalo na umegawanywa katika sehemu kuu nne, ambazo ni uwezo, udhaifu, fursa na changamoto zilizopo. Uchambuzi huu unafanyika kwa lengo la kufanya utekelezaji wa mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii ufanikiwe.

**Uwezo** ni mambo yaliyo nchini ambayo yanaipa nchi nguvu ya kufanya mambo vizuri na kwa ufanisi, wakati **Udhaifu** ni mambo yanayoifanya nchi ishindwe kufanya shughuli zake vizuri. **Fursa** ni yale mambo ambayo nchi inayo au inaweza kuyapata nje na ingeweza kuyatumia kwa manufaa yake, na mwisho **Changamoto** ni yale mambo ambayo yanaweza kuleta matatizo ama kurudisha nyuma shughuli za kimaendeleo nchini.

## Jedwali 4. Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

| Uwezo | Udhaifu |
|---|---|
| • Ukuaji imara wa uchumi<br>• Idadi kubwa ya vijana(nguvu kazi ya kutosha )<br>• Upatikanaji wa ardhi yenye rutuba na maliasili nyingi za aina mbalimbali<br>• Nchi ipo pazuri kijiografia (bandari, bahari, maziwa n.k)<br>• Umoja wa kitaifa, amani na maelewano, lugha moja, mshikamano wa kweli.<br>• Miundombinu imeboreshwa na mtandao wa mawasiliano umesambazwa pote nchini.<br>• Elimu kwa wote na ongezeko la vyuo vya elimu ya juu.<br>• Afya: ongezeko la hospitali za kisasa (kama vile hospitali ya moyo ya Jakaya Kikwete) | • Umasikini – idadi ya masikini ni kubwa na tofauti kati ya wenye nacho na wasionacho inaongezeka<br>• Teknolojia na viwanda – elimu ndogo ya teknolojia, uwekezaji mdogo kwenye teknolojia, uwekezaji mdogo wa teknolojia kwenye viwanda vidogo na vya kati, utegemezi mkubwa kwenye njia za asili za kilimo.<br>• Sekta binafsi na biashara – ni dhaifu kwa upande wa wazawa na kampuni za wazawa ni chache katika biashara za kimataifa.<br>• Soko la ajira – wasio na ajira ni wengi pamoja na wasomi wa vyuo vikuu wasio na ujuzi wa kutosha kulingana na soko la ajira<br>• Elimu – thamani ya elimu ni ya chini (vitendea kazi duni,ufundishaji duni)<br>• Afya – mfumo dhaifu wa utoaji huduma (kwa mfano, ukosefu wa wataalamu wenye ujuzi na weledi, na bima ya afya ipo chini sana, haijawafikia wengi)<br>• Nishati na maliasili - upatikanaji wa umeme usio wa uhakika na matumizi mabaya ya maliasili.<br>• Hali ya uchumi – ukosefu wa dira na itikadi ya kiuchumi,utekelezaji hafifu wa mbinu bora za zamani. |
| **Fursa** | **Changamoto** |
| • Soko na biashara – makubaliano kati ya nchi na nchi na ushirikiano wa kikanda kama vile, jumuiya ya afrika mashariki, jumuiya ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC), shirikisho la biashara afrika,mpango wa makubaliano ya kibiashara na marekani kuhusu mazao ya kilimo na madini.<br>• Kubadilishana teknolojia baina ya mataifa<br>• Mawasiliano - gharama ndogo ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika<br>• Huduma za afya – kuna wadau wa afya kwa ajili ya kuboresha huduma za afya<br>• Mitaji – uboreshwaji wa soko la mitaji (mfano, M-PESA inavyotumika barani afrika<br>• Hali ya ushindani – ongezeko la bidhaa za Tanzania (hasa mazao ya kilimo) inayotokana na ongezeko la watu kikanda.<br>• Baadhi ya nchi jirani hazina bandari<br>• Mifano ya kuigwa – Uwepo wa mifano inayoweza kuigwa inayohusu uchumi jamii inayoweza kutekelezwa nchini Tanzania. | • Masoko huria na biashara – uwezo wa makampuni makubwa ya kimataifa dhidi ya biashara za wazawa.<br>• Teknolojia – ushindani mdogo kwenye ulimwengu unaobadilika haraka kiteknolojia.<br>• Mazingira – hali ya hewa isiyoridhisha na mabadiliko ya tabia nchi yanayotokea<br>• Hali ya ushindani wa kibiashara: mazingira mazuri kwenye nchi zingine<br>• Hali ya kisiasa isiyotulivu katika nchi zinazopakana na Tanzania. |

# 4.0. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii nchini Tanzania

Baada ya kufanya tathmini juu ya hali ilivyo nchini Tanzania, muhtasari huu unapendekeza mfumo wa uchumi ambao utaisaidia Tanzania kuweza kufanikisha mipango yake ya kuwa na maendeleo shirikishi na endelevu. Aidha, mfumo wa uchumi unaopendekezwa ni wa Soko Jamii kwa kuwa unaendana na hali halisi ya Tanzania.

**Nini dhamira ya Uchumi wa Soko Jamii?**
Dhamira ya mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii ni kuwa na taifa imara lenye ukuaji wa uchumi ambao ni endelevu na jumuishi ambao unawezesha ushiriki wa watu wote na maendeleo kwa wote. Mfumo huu wa uchumi unaipeleka Tanzania katika mafanikio ya kiuchumi kwa kufuata miongozo ya kimaadili na mikakati iliyoelezewa vizuri katika sekta mbalimbali.

**Ni namna gani mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii utafikia malengo yake?**
Kazi ya mfumo wa Uchumi wa soko Jamii ni kuzielekeza shughuli zote za kimaendeleo za nchi kwenye uchumi jumuishi ambapo biashara huria na ushindani vinakuwa kwenye mizania ya usawa. Usawa huu unatokea serikalini na kwa mtu mmoja mmoja ambao ndio kitovu cha uamuzi na matendo ya kila Mtanzania.

**Ni tunu zipi zinazosimamia mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii?**
Kuna tunu 11 za msingi zinazosaidia utekelezwaji wa mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. Tunu hizi zinaweza kuwekwa kwenye kifupisho cha “KWA NCHI YETU” kama zinavyoelezewa hapa chini.

**K** **Knowledge**, ufahamu na ujuzi wa mambo muhimu kuhusu shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na ziada kuuzwa nje huongeza ufanisi na kuzuia gharama zisizo za lazima. Ujuzi wa kitaalamu pia ni msingi wa kuwa na nguvukazi yenye uwezo. Nguvukazi iliyoelimika ni chanzo cha ubunifu na uwepo wa huduma bora. Mbali na haya, ujuzi na uelewa juu ya namna masoko yanavyofanya kazi na kuwa na taarifa muhimu kuhusu, kwa mfano, bei za bidhaa, kiasi na aina ya bidhaa inayohitajika sokoni, wazalishaji wa bidhaa husika, hali ya ushindani n.k ni vitu muhimu kuwezesha uchumi wa soko uwe na ufanisi.

- **W** **Wisdom**, hekima ni jambo muhimu katika siasa kufanikisha uwepo wa utawala bora. Hekima huishinda rushwa na kuhakisha kuwa wanasiasa wanatengeneza mikakati ya muda mrefu ya uwajibikaji na endelevu.

- **A** **Accountability**, uwajibikaji unahakikisha kuwa wadau wote wanafanya kazi kikamilifu na kwa ufanisi ili kufikia maendeleo yenye usawa. Ni muhimu kuzingatia utawala wa sheria, haki ya mali binafsi na utaratibu wa kidemokrasia. Mfumo imara wa mahakama usioingiliwa pamoja na uchaguzi huru na wa haki ni sehemu pia ya uwajibikaji.

- **N** **Nation first,** Uzalendo ni ile hali ya kulipenda taifa lako na kujivunia. Watanzania wanaweza kujivunia utajiri wa kitamaduni, jamii yenye amani na uwepo wa rasilimali nyingi. Wananchi wanapaswa kujengewa uwezo na kufahamu uwepo wa haya yote ili kuwa na taifa imara na huru. Ingawa uzalendo hauna maana ya kujiondoa au kutoshiriki. Mtazamo finyu na ule wa ndani zaidi unaweza kujenga taifa lililodumaa na kuathiri maendeleo ya kipindi kirefu cha baadaye. Kwa hiyo, taifa linahitaji kujiamini na kuweka uwiano mzuri kati ya uwezo wake na mataifa mengine duniani.

- **C** **Community**, Jumuiya inatoa nafasi ya mshikamano, kufanya kazi kwa pamoja na kusaidiana ili kufikia mafanikio. Pia ni sehemu ambayo watu wanaweza kupata utambulisho wa pamoja, kulingana na yale yanayowatofautisha au wanayofanana. Katika dunia ya sasa ambayo kutofahamiana kunaongezeka, dhana ya jamii inaweza kutumika kuunganisha tofauti zilizopo. Kwa sababu haiwezi kupelekea ubaguzi na uvunjifu wa haki za kiraia, jumuiya ni kiungo muhimu ili kuwa na jamii iliyo na umoja na amani.

- **H** **Human dignity**, utu wa mtu ni lazima uheshimiwe na wanasiasa pamoja na wadau wa uchumi ili kuhakikisha kuwa maisha ya Watanzania, mazingira yao pamoja na taasisi zao zinalindwa kikamilifu. Zaidi ya yote, nguzo hii ya utu ni lazima imwezeshe kila mtu kuishi maisha yenye staha.

- **I** **Integrity**, uadilifu: wadau wote kupitia mfumo huu wa kiuchumi wanapaswa kuzingatia uaminifu. Ili kusimamia na kulinda wengine dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka, taasisi huru zinapaswa kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoathiriwa na wanasiasa na wadau wengine kwenye uchumi.

- **Y** **Youth**, Vijana: uwepo wa vijana kwenye jamii na nguvu kazi kubwa kwenye soko la ajira kuna tafsiri kubwa mbili, tafsiri ya fursa na changamoto kwa taifa. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania unawaweka vijana kama sehemu muhimu, kama taifa jipya na viongozi wa baadaye. Kwa hiyo, ili kuwa na mafanikio ya nchi siku za usoni, ni vyema kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu bora, kukidhi mahitaji ya lazima na kuruhusu watoto wakue vizuri katika uwepo wa huduma nzuri za afya na mazingira rafiki ya watoto na kijana kujiendeleza.
- **E** **Evaluation**, tathmini ya sera za maendeleo na shughuli zote za kiuchumi ni jambo muhimu ili kufanya uamuzi sahihi, kujifunza kulingana na makosa na kutekeleza mbinu mpya kuleta mageuzi. Wadau wote muhimu kwenye uchumi lazima wafanye tathmini ya matokeo ili kujua uwezo na mapungufu yao. Ili kuwa na ufanisi, kufanyika kwa tathmini lazima kuambatane na kuchuka hatua kwa wakati na kufanya maamuzi yenye tija.
- **T** **Transparency**, Uwazi katika kufanya maamuzi na utekelezaji wake, unapaswa kuzingatiwa ili kuleta ufahamu miongoni mwa wadau. Hii ni pamoja na kuelewa majukumu yao. Uwazi unaondoa mikanganyiko na hii ni nguzo muhimu zaidi katika utawala wa kidemokrasia.
- **U** **Unity, Umoja / Mshikamano,** hii ni tunu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na huwezesha nchi kuwa na mazingira rafiki kwa uwekezaji na biashara za nje. Umoja huu wa kitaifa unafaa utumike katika kuleta mshikamano na uhamasishwe bila kuchoka.

## 4.1. Mikakati


Ili kusukuma maendeleo ya kiuchumi mbele na kufikia maendeleo yenye usawa, na hatimaye kupunguza umasikini kwa kiwango kikubwa, mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unapendekeza mikakati mbalimbali. Ukuaji wa kiuchumi pekee hautakuwa na tija iwapo hakuna mikakati madhubuti katika maeneo ya kisera na kuhakikisha kila mwananchi na mdau anaelewa ni kwa namna gani tunaweza kufikia uchumi shirikishi na maendeleao endelevu. Misingi, tunu na mikakati ya mfumo wa Uchumi Jamii kwa pamoja itasaidia kusukuma mbele maendeleo ya taifa letu.

Mchanganuo ufuatao unaonesha maeneo muhimu ya kisera ya mfumo wa Uchumi Jamii. Pamoja na uchambuzi wa hali ya nchi kama ulivyobainishwa katika sura ya tatu, changamoto mbalimbali za kisera zitabainishwa, mikakati madhubuti na mifano halisi itapendekezwa ili kutoa mwogozo au uelekeo.

## Mfumo wa Uchumi

Mfumo wa Uchumi Jamii unafaa uratibiwe ipasavyo. Hii ni pamoja na kuweka malengo kwa kila sekta na kuhakikisha kila mdau anatambua majukumu yake katika kujenga uchumi wa taifa. Mipango ni lazima ifanyike kwenye ngazi zote; kutoka ngazi ya chini mpaka ile ya kitaifa.

**Kielelezo 6: Vipengele vya Mfumo wa Uchumi**




## Kuweka mfumo wa kisheria unaoaminika

**Mkakati:** Kanuni zinapaswa kuweka wazi mgawanyo wa kazi. Majukumu ya serikali na sekta binafsi ni muhimu yakafahamika kwa uwazi. Pia taasisi za umma na zile za binafsi zinapaswa kupewa majukumu. Mfumo huu utahakikisha kuwa ugatuzi wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda kwenye taasisi zingine unaimarisha uhuru wa taasisi hizi na mapambano dhidi ya rushwa na kurahisisha utendaji kazi.

## Kuwalinda wananchi wa Tanzania na kuheshimu utu na ubinadamu wao

**Hali halisi:** Mara nyingi wananchi wa Tanzania hawalindwi wanapokuwa kwenye mazingira ya kazi. Hii inajumuisha taratibu mbovu za kazi, ajira za watoto na ukandamizaji wa namna mbalimbali.

**Mkakati:** Serikali inapaswa kuhakikisha taratibu za kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa mahakama zinazingatiwa. Taasisi zinazopigania haki za binadamu zinapaswa kuungwa mkono

ikiwa ni pamoja na kuruhusu taasisi za kijamii kufanya kazi kwa uhuru na weledi.

## Kutoa huduma bora za jamii

**Hali halisi:** Pamoja na ukweli kuwa bidhaa na huduma za umma zipo nchini, huduma hizi si za kutegemea. Wakati mwingine serikali inapuuza huduma hizi au kuzitoa kwa kiwango kisicho na ubora stahiki. Mgawanyo wa huduma hizi bado sio wa kuridhisha.

**Mkakati:** Maeneo muhimu zaidi ya huduma hizi za umma ni pamoja na afya, elimu na miundombinu. Ni vyema serikali ikajikita katika kutoa na kusimamia huduma hizi. Katika kufanya hivyo ubaguzi wa aina yoyote ile ni lazma ukemewe.

### Mfano wa mkakati: Huduma ya afya kwa wote

Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unapendekeza mfumo ambao wananchi wote wanaweza kupata huduma za msingi za afya. Gharama hizi za matibabu zinachangiwa na wananchi wote wanaofanya kazi. Michango hii inakusanywa pamoja na kuhudumia wale wanaopata maradhi ikiwa ni pamoja na wasiojiweza kama watoto, wazee na wasioajiriwa. Ni muhimu kwa serikali kusimamia mfumo huu na kuhakikisha kuwa unafanya kazi sawa sawa na kuusaidia inapobidi.

## Kuheshimu na kulinda mali binafsi

**Hali halisi:** Umiliki wa mali binafsi ni jambo muhimu na linachochea wananchi kushiriki katika uzalishaji mali na kupata kipato. Kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya chini katika kulinda mali binafsi kwa kuwa bado mali za wawekezaji binafsi zinataifishwa. Wadau wa sekta binafsi hawana nguvu ya kusema lolote juu ya hili. Usajili wa mali binafsi ni wa gharama kubwa na huchukua muda mrefu ukilinganisha na nchi nyingine.

**Mkakati:** Ili mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii uweze kufanya kazi vizuri ni muhimu kuwepo na ulinzi wa haki milki ya ubunifu na mali.

Haki ya kumiliki mali ni lazma iheshimiwe kisheria na mfumo wa mahakama ulio huru na wa haki. Usajili wa haki milki ni vema ukarahisishwa. Lazima kuwepo na makubaliano ya wazi juu ya haki milki ili kulinda watu binafsi katika soko.

### Kutoa motisha katika kufanya biashara

**Mkakati:** Motisha kutoka serikalini ni muhimu katika maendeleo ya kiuchumi. Kwa mfano serikali inaweza kutoa ruzuku kwenye maeneo mbalimbali au kupunguza kodi kimkakati ili kuhamasisha uwekezaji kwenye baadhi ya maeneo kama vile viwanda.

## Mfumo wa Uchumi Mkubwa

Maendeleo ya uchumi mkubwa huchangiwa na mipango ya muda mrefu na usimamizi madhubuti wa uchumi. Hii inaelezwa vizuri zaidi kwenye maeneo ya kisera yafuatayo:

### Hakikisha kuna sera ya fedha inayojitegemea

**Hali halisi:** Benki kuu ya Tanzania ndio benki inayosimamia na kudhibiti fedha za nchi yetu pamoja na mfumuko wa bei. Benki kuu ya Tanzania ilikuwa huru zaidi katika utendaji wake kupitia sheria mpya ya mwaka 2006 ingawa bado kuna changamoto ya kuingiliwa na maamuzi ya kisiasa. Serikali inateua watendaji wa Benki kuu na kupanga mishahara na mafao yao ya uzeeni, hii inasababisha benki hii kutokuwa na uhuru wa kujitegemea.

**Mkakati:** Ni lazima Benki Kuu ya Tanzania iwe huru na iondokane na ushawishi wa kisiasa. Mchakato wa kuwapata watumishi wa benki kuu ya Tanzania unapaswa kuzingatia ujuzi na ubobezi. Wanaoomba nafasi hizo ni vema wakafanyiwa usaili ili kupata wasimamizi na watumishi makini wa taasisi hii muhimu. Taratibu zinapaswa kusimamiwa vizuri kuhakikisha benki kuu inaweza kupambana na athari za changamoto mbalimbai za masoko ya fedha.

## Hakikisha kuna uchumi imara


**Hali halisi:** Tanzania ilijiunga na Shirika la Fedha Duniani (International Monetary Fund-IMF) tangu mwaka 1962. IMF inalenga katika kuimarisha ushirikiano wa kifedha kimataifa na kuhakikisha masuala ya fedha yanakua imara ili kufikia ukuaji endelevu wa kiuchumi duniani. Kulingana na takwimu za shirika hili, Tanzania imeendelea kuwa na kiwango cha chini cha mfumuko wa bei, thamani ya shilingi imeendelea kuimarika na riba za mikopo zimeimarika pia.

**Mkakati:** Kuhakikisha kuwa shughuli za kiuchumi zinaendeshwa kwa kutumia mapato ya ndani na hivyo kupunguza mikopo ya nje. Usimamizi madhubuti wa uchumi utahahakisha nchi inajenga uchumi imara na hivyo kuvutia wawekezaji na biashara.

### Mfumo wa Soko

Soko huru lenye ushindani ni moja ya nguzo muhimu za mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. Ushindani wa kibiashara ni muhimu katika kuimarisha biashara na kuongeza ufanisi na hivyo kupelekea kuingia kwenye biashara ya kimataifa. Kwa ujumla ushindani wa kibiashara ni muhimu kuwa huru ili kuongeza uzalishaji lakini vilevile uratibu wa biashara hizi ni muhimu ili kuleta ushindani wenye usawa. Mfumo mpya wa soko utaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi nchini Tanzania.

**Kielelezo 7: Soko Katika Mfumo wa Uchumi Jamii**



## Imarisha ushindani na masoko huru

**Hali halisi:** Uwiano mzuri kati ya soko huria na udhibiti wa serikali huchagiza maendeleo ya viwanda. Kwa nchi ya Tanzania sekta binafsi haikui ipasavyo kwa sababu ya kukosekana kwa uwiano huu. Kukithiri kwa biashara kubwa za kimataifa kunavunja hamasa ya wawekezaji wadogo. Nchi ina baadhi ya bodi za usimamizi kama bodi ya pamba zinazotoa bei elekezi.

**Mkakati:** Ni muhimu kwa bodi za usimamizi kufanya kazi kwa kuzingatia usawa na ukuaji wa masoko. Mfumo wa Uchumi Jamii utaondoa bei elekezi na hivyo kuruhusu soko kustawi na wadau wake kuwa na ushindani wenye tija.

## Simamia masoko na hakikisha kuna haki na usawa

**Hali halisi:** Makampuni makubwa yanayohodhi mwenendo wa soko yapo nchini Tanzania kwenye sekta kama za nishati na usafiri wa anga. Tume ya ushindani Fair Competition Commission-FCC inapaswa kuhakikisha kunakuwa na mfumo imara wa soko huru na ushindani wenye ufanisi kwa wadau wote kwenye biashara. Tume inawajibika kupambana na mienendo isiyo ya haki na isiyofaa kwenye soko kama vile kuungana kusikofaa na umiliki wa soko. Hata hivyo tume hii inashindwa kuwa na meno kwa kuwa teuzi za watumishi wake na mishahara na posho zao zinakuwa na misukumo ya kisiasa. Tume hii inawajibika moja kwa moja kwa Rais wa nchi.

**Mkakati:** Ni muhimu tume ya ushindani kufanya kazi kwa uhuru. Tume hii inapaswa kuhakikisha nguvu ya soko isiyo na uwiano wenye tija inadhibitiwa, ushirikiano wa wafanyabiashara wa ngazi ya chini lazima uruhusiwe, kwa kadiri inavyowezekana, ili kufanya wadau washindane kwa kiwango cha juu na kuongeza tija na uzalishaji wa bidhaa na huduma zenye kiwango bora.

### Hakikisha taarifa sahihi za mwenendo wa soko zinawafikiwa wadau wote katika soko

**Hali halisi:** Kwa sasa ni vigumu wadau kupata taarifa sahihi za masoko kwa kuwa vyombo vya habari nchini haviko huru kutoa taarifa hizo.

**Mkakati:** Taarifa kuhusu mambo mbalimbali zinapaswa kuwafikia wadau wote kupitia vyombo vya habari vyenye nguvu na huru. Panapokuwa na uhuru wa kujieleza kwa watu binafsi na vyombo vya habari, maendeleo ya kiuchumi hupatikana kwa kasi kwa kuwa wadau wote hupata taarifa na elimu sahihi juu ya fursa mbalimbali za uwekezaji na masoko. Pia wawekezaji hutegemea vyombo huru vya habari kufanya machaguo ya uwekezaji kwa kuwa uhuru wa habari huongeza imani kwa serikali pamoja na mfumu wa kiuchumi kwa wananchi husika. Sheria za sasa za vyombo vya habari zinapaswa kuboreshwa ili kutoa uhuru zaidi wa kujieleza.

**Mfumo wa Biashara**

Wadau hukutana kwenye masoko ili kubadilishana bidhaa na huduma. Ili kuhakikisha makampuni na biashara zinaendelea kushamiri, ni vyema kuhakikisha kunakuwa na mikakati ya kuimarisha sekta binafsi. Ni muhimu kukawa na ushindani unaozingatia usawa kwa washiriki wote.

### Imarisha sekta binafsi

**Hali halisi:** Sekta binafsi nchini bado ni changa na biashara nyingi zinashindwa kuendelea kwa sababu ya changamoto nyingi za usajili na mambo ya kodi ingawa zipo baadhi ya taasisi kama Taasisi ya Biashara, Viwanda na Kilimo (Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture) ambazo zinasaidia kutoa taarifa na elimu juu ya haki ya mjasiriamali. Mbali na hayo, bado kuna makapuni yaliyohodhi biashara kwenye sekta muhimu kama vile nishati na usafiri wa reli. Hii inatokana na ukweli kuwa nchi ya Tanzania imetaifisha na kumiliki makampuni kama ya reli n.k.

**Mkakati:** Ni vema kukawa na mazingira rafiki kwa uwekezaji wa sekta binafsi ili kurahisisha uanzishaji wa biashara. Ni muhimu kukawa na taratibu za wazi na zinazoeleweka kwa wawekezaji na serikali iondokane na kutaifisha na kuingilia uendeshaji wa soko isipokuwa pale inapobidi.

## Saidia uanzishaji biashara ndogo na za kati (SMEs)

**Hali halisi:** SMEs ni biashara zenye idadi ya wafanyakazi kati yaa 50 mpaka 250. Kwa sasa biashara hizi zinakumbana na changamoto ya kodi na kukosa msaada wa serikali. Imekuwa ni vigumu sana kukukua kwa biashara hizi kwa sababu ya mitaji midogo, kodi na gharama kubwa zinazohitajika wakati kuanzisha biashara.

**Mkakati:** Uanzishwaji wa biashara hizi unapaswa kuwa na taratibu rahisi ili kuweza kunufaika na ubunifu na ongezeko la uwekezaji wa wafanyabiashara hawa. Kwa mfano wafanyabiashara hawa wadogo na wa kati wanaweza kupewa msamaha wa kodi pale mwanzoni mwa biashara wanapokuwa hawajaanza kupata faida. Hata hivyo ni vyema msaada kwa wafanyabishara hawa ukaratibiwa kwa umakini ili kutoruhusu udanganyifu. Vilevile serikali inaweza kuwapatia elimu juu ya uendeshaji wa biashara na teknolojia muhimu na kuhakikisha kila mjasiriamali mdogo na wa kati ana uelewa wa sheria mbalimbali.

### Mfano: Motisha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati

Mfumo wa Uchumi Jamii unapendekeza punguzo la kodi kwa mwaka wa kwanza wa biashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Vilevile serikali inaweza kutoa motisha kwa makampuni yanayofanya jitihada za kutunza mazingira wakati yanaendesha biashara zake.

## Hakikisha kuna majadiliano na wadau mbalimbali

**Hali halisi:** Shirikisho la wafanyakazi la Zanzibar na Tanzania bara hushirikiana kwa pamoja katika kujadili sera na mipango mbalimbali. Vilevile vyama vya waajiri vipo kwa ajili kutoa msaada wa miongozo ya kisheria, elimu na ushauri kwa

wanachama mbalimbali kupitia makongamano na vikao juu ya mambo ya kiuchumi yanayojitokeza nchini na kwingineko.

**Mkakati:** Mazungumzo kati ya sekta binafsi na ile ya umma yatasaidia kubadilishana mawazo na kuweza kubainisha maeneo ya kufanyiwa kazi kwa pamoja. Wadau wa sekta binafsi wanapaswa kuungana ili kuwa na nguvu na kwa pamoja waweze kutetea maslahi yao.

## Mfumo wa Kodi

Mfumo wa kodi au sera ya fedha ni muhimu katika uzalishaji wa bidhaa na uendeshaji wa shughuli za kiserikali. Ni muhimu kukawepo viwango na aina za kodi ambazo zitaisaidia serikali kujiendesha yenyewe bila kutegemea misaada kutoka nje. Wakati huo huo kodi hizi hazipaswi kuwa kubwa mno kiasi cha kumwathiri mlipa kodi. Mfumo wa Uchumi Jamii unapendekeza mfumo wa kodi ambao ni rafiki kwa biashara na wenye kuwasiadia wananchi wazawa.

### Anzisha sheria na kanuni ambazo ni rafiki kwa uwekezaji

**Hali halisi:** Kiwango cha kodi kilichopo nchini kimelalamikiwa sana na wawekezaji na wajasiriamali. Kumekuwa na ongezeko la tozo na kodi kwenye baadhi ya maeneo kama vile kuhamisha fedha kwa njia ya mitandao ya simu, mabenki, utalii na huduma za usafirishaji wa shehena kupitia nchini.

**Mkakati:** Sheria za kodi zilizo rafiki kwa uwekezaji zitasaidia kuvutia biashara na kukuza sekta binafsi. Hii ni pamoja na kutoa motisha kwa biashara zinazoanza na kwa makampuni yanayozingatia utunzajia wa mazingira. Motisha za aina hii zitasaidia kukuza uwekezaji na uzalishaji.

### Kakikisha kuwa mfumo unaeleweka kwa wadau

**Hali halisi:** Viwango vya kodi nchini Tanzania havitabiriki kwa kuwa hubadilika mara kwa mara. Vile vile mfumo wa kodi si rahisi


kueleweka kwa wananchi ambao hawana uelewa mpana wa somo la uchumi. Kutokana na ugumu wa mfumo huu wa kodi, makosa, ukwepaji kodi na udanganyifu hujitokeza.

**Mkakati:** Ni vyema kukawa na mfumo wa kodi unaoeleweka ili kuzuia makosa katika ukusanyaji kodi. Taarifa mbalimbali zinapaswa kupatikana kwa urahisi kwa kila anayezihitaji na mwisho ni vyema nchi ikawa na mipango na mikakati ya muda mrefu ili kuwa na mfumo wa kodi unaotabirika na usiobadilika mara kwa mara. Hii itasaidia kuongeza imani na kuvutia wawekezaji.

## Rekebisha viwango vya kodi kwa uwiano

**Mkakati:** Muundo wa kodi unapaswa kuzingatia usawa na haki kwa jamii. Mfumo wa kodi unapaswa kuendana na kipato cha mlipa kodi ili kila mmoja alipe kulingana na kipato chake. Kwa njia hii kila mwananchi mwenye kipato atachangia katika pato la taifa.

**Kielelezo 8: Uwiano wa Kodi na Kipato**




## Ongeza ufanisi katika ukusanyaji kodi

**Hali halisi:** Nchini Tanzania kodi zinakusanywa na serikali za mitaa na serikali kuu. Kwa kipindi kirefu kumekuwa na changamoto

kwenye ukusanyaji wa kodi kutokana na sababu mbalimbali. Ugumu wa kuwatambua walipa kodi, uelewa mdogo wa Watanzania juu ya kodi mbalimbali na usimamizi mbovu wa makusanyo ya kodi zimekuwa ni baadhi ya changamoto zinazopelekea kutofikia malengo ya makusanyo ya kodi.

**Mkakati**: Serikali inapaswa kuongeza ukusanyaji kodi kwa kuboresha mfumo wa makusanyo ya kodi. Mfumo wa Uchumi Jamii unapendekeza elimu ya kutosha itolewe kwa walipa kodi wote, wananchi watambue aina za kodi na namna ya ulipaji wake. Serikali inapaswa kuweka utaratibu mzuri wa kuyafatilia makampuni makubwa ili kuhakikisha yanalipa kodi stahiki. Kila mlipa kodi anatakiwa apatiwe mashine ya kodi, yaani EFD, ili kutunza kumbukumbu ya taarifa za kodi na mapato.

### Hakikisha kunakuwa na mfumo mzuri wa mgawanyo wa mapato

**Hali halisi:** Serikali kuu kupitia TRA ndiyo inayokusanya kodi kwa kiwango kikubwa. Makusanyo ya moja kwa moja ya serikali za mitaa ni kiwango kidogo. Serikali kuu hugawanya mapato hayo kwa serikali za mitaa ambazo ndizo zenye jukumu la kutoa huduma za jamii kwa wananchi. Mfumo wa mgawanyo wa mapato haya kwa serikali za mitaa hauko uwazi. Si mara zote inafahamika ni wadau gani wamepewa fedha ya kodi na ni sababu zipi zimepelekea mgawanyo huo.

**Mkakati:** Ni lazma kuwepo na mpango wa nchi wa makusanyo ya kodi ambao unazipa serikali za mitaa madaraka zaidi juu ya makusanyo na matumizi ya kodi. Hii inatokana na ukweli kuwa serikali za mitaa ndizo zinazowajibika moja kwa moja kwa wananchi. Serikali za mitaa zikipata madaraka zaidi itaongeza motisha ya kuwahudumia wananchi na hii itakuwa chachu ya maendeleo kwa ujumla.

### Mfumo wa Kimataifa

Uhusiano wa kikanda na kimataifa unaweza kutumika kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi.

## Jenga uwezo kupitia ushirikiano wa kimataifa

**Hali halisi:** Tanzania ina washirika wengi waliotayari kuisaidia kifedha na kiufundi ili kufikia malengo yake. Mashirika haya ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Benki ya Dunia kupitia mkakati wa kusaidia nchi na Shirika la Biashara Duniani. Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa juu ya Forodha na Biashara (GATT) mwaka 1961 na hivyo kuwa mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) tangu mwaka 1995, kumeisaidia Tanzania kuingia kwenye soko la kimataifa. Vilevile balozi na taasisi mbalimbali za misaada zinasaidia utekelezaji sera za miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

**Mkakati:** Ni lazima nchi ya Tanzania ijenge uwezo kupitia mahusiano ya kibiashara na mikataba ya kimataifa. Kwa mfano kupitia umoja wa nchi za Afrika Mashariki kuna fursa za masoko ya bidhaa na ajira kwa wananchi wake. Pia ipo fursa ya kuboresha maisha kupitia mashirikiano ya kisiasa, kiuchumi na kimazingira. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unahamasisha kuanzishwa kwa sarafu moja itakayotumika na nchi za Afrika Mashariki. Hii itasaidia kuimarisha thamani shilingi na kuwezesha nchi ya Tanzania kuweza kushindana kimataifa.

### Mfumo wa Kijamii

Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unajumuisha taratibu nyingi za hifadhi ya jamii. Lengo kuu ni kuhakikisha kila mwana jamii anapata huduma stahiki. Mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

## Toa mfumo rahisi na wa wazi wa hifadhi ya jamii

**Hali halisi:** Kwa sasa mfumo wa hifadhi ya jamii unajumuisha mafao mbalimbali ikiwemo ya uzeeni pamoja na bima ya afya. Kuna mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii inayoendeshwa kwa taratibu tofauti tofauti na hivyo kuleta mkanganyiko. Mafao yanayotolewa na mifuko hii hutofautiana pia. Kumekuwepo na juhudi za kuunganisha mifuko hii ili iweze kuendeshwa

kwa taratibu zinazofanana, ingawa kumekuwa na wanaopinga hatua hii.

**Mkakati:** Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unahamasisha mfumo wa hifadhi ya jamii wenye kukidhi vigezo vya kimataifa. Mfumo wa bima ya afya na mafao ya uzeeni ni kati ya mambo yanayoweza kutolewa kwa mfumo mmoja. Kwa kufanya hivyo Watanzania wengi wataelewa mfumo wa uendeshaji wa mifuko hii na watafaidika na huduma ya hifadhi ya jamii na hatimaye kuweza kupunguza umasikini.

**Mfano wa mkakati wa hifadhi ya jamii kwa wote**

Mfumo wa hifadhi ya jamii unahakikisha umasikini unapungua kwa kuwa huduma nyingi za afya zitapatikana bila malipo ya papo kwa hapo. Vile vile mfumo huu utasaidia wale waliopoteza ajira, waliojifungua na wale wenye magonjwa mbalimbali kuweza kupata matibabu na hatimaye kurejea katika hali ya kuweza kuendelea na ujenzi wa Taifa.

## Hakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma

**Hali halisi:** Watanzania wengi hawako katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kuwa uanachama wa mifuko hii ni wa lazima kwa wale wote waliopo kwenye ajira rasmi. Wananchi walio kwenye ajira isiyo rasmi hawalazimiki kujiunga na mifuko hii. Umasikini uliokithiri na ukosefu wa elimu unasababisha watu wengi wasijiunge na mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Mkakati:** Ni muhimu kwa kila mwananchi achangie mfuko wa hifadhi ya jamii kulingana na kipato chake. Kwa wale ambao hawana uwezo wa kuchangia, mfumo utawapatia fursa ya kupata huduma za msingi kwa gharama nafuu. Vilevile elimu inapaswa kutolewa kwa wananchi wote juu ya hifadhi ya jamii.

## Hakikisha elimu bora ya msingi inapatikana kwa wote

**Hali halisi:** Mfumo wa elimu bila ada katika shule za msingi umewezesha watoto wengi kupata nafasi ya kwenda shuleni. Hata hivyo kiwango cha ubora wa elimu kinachotolewa ni cha chini na

mazingira na vifaa vya kufundishia ni hafifu. Shule nyingi hazina mazingira rafiki kwa watoto wenye ulemavu wa aina mbali mbali. Changamoto nyingine ni mimba za utotoni pamoja na gharama nyingine za kupata elimu (mbali na ada) kuwa kubwa.

**Mkakati:** Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unafanya kazi ya kuongeza ubora wa elimu na unapendekeza kuwekeza zaidi kwenye vifaa vya kufundishia. Walimu wanaoajiriwa wanapaswa kupewa elimu na maarifa juu ya mitaala ya kufundishia na wapate mishahara yenye kukidhi mahitaji yao ya msingi. Mabadiliko yoyote ya mitaala ni vyema yakafanyiwa utafiti wa kina kwa kushirikiana na wadau wote wa elimu. Mazingira ya shule yanatakiwa kuboreshwa ili kutoa nafasi ya elimu bora kwa watoto wa kike na wenye ulemavu na changamoto mbalimbali. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii huchukulia elimu kama uwekezaji hivyo unahakikisha wawoto wanapata mahitaji muhimu yanayowawezesha kusoma bila shida. Msaada wa nchi za nje unaweza kuhitajika kuyafanya yote haya.

## Boresha mafunzo ya vyuo na taasisi za elimu ya juu kuendana na mahitaji ya soko la ajira

**Hali halisi:** Elimu ya juu nchini hutolewa kwenye taasisi kuu tatu; vyuo vikuu, taasisi za vyuo vya ufundi na vituo vya elimu ya ufundi (VETA). Idadi ya vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu imeongezeka, lakini mitaala ya ufundishaji haizingatii kutoa ujuzi kwa wahitimu. Vile vile wahitimu hawa wanapata changamoto ya uelewa mdogo wa lugha ya kiingereza ambayo ndiyo hutumika kutolea mafunzo.

**Mkakati:** Elimu ya vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu inapaswa kuwajengea wahitimu ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira ili kuwawezesha kuajiriwa. Mitaala hii inapaswa kujumuisha mafunzo kazini ili wanafunzi waweze kupata mafunzo kwa vitendo. Wanafunzi wanapaswa kuelimishwa juu ya machaguo ya kozi mbalimbali zinazofundishwa ili waweze kufanya machaguo sahihi. Taasisi na vyuo vya ufundi viwekewe mkazo

zaidi kwani hivyo ndivyo hutoa ujuzi mbalimbali unaohitajika kwenye soko la ajira. Majadiliano ya mara kwa mara baina ya wadau wa elimu kama wanasiasa, wakufunzi na wengineo yanapaswa kuwa endelevu ili kupata matokeo chanya.

## Sekta ya Kilimo na Mazingira

Sekta ya kilimo ni suala kubwa kwenye ajenda ya maendeleo ya uchumi kwa Tanzania. Sekta hii inaajiri takriban therithi mbili ya wananchi wote, kuanzia wakulima na hata viwandani kwa kuwa kilimo ndicho chanzo cha malighafi za viwandani. Hii ina maana kuwa kilimo ni sekta muhimu vijijini na kinachangia kuboresha kiwango cha maisha kwa watu wake.

### Anzisha maendeleo endelevu

**Hali halisi:** Tanzania ina mikakati michache juu ya uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali.

**Mkakati:** Kujumuisha sera ya maendeleo endelevu na mpango wa maendeleo ya mazingira kwenye sera za kijamii na kiuchumi itaisaidia nchi ya Tanzania kupiga hatua ya maendeleo. Hii ni pamoja na kupunguza uchafuzi wa mazingira, kupunguza utegemezi wa nishati ya mafuta na kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali.

### Ongeza hamasa juu ya utunzaji wa mazingira

**Hali halisi:** Mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi yamekuwa changamoto kubwa sana kwenye sekta ya kilimo. Kuongezeka kwa joto duniani na tabia zisizofaa kwa mazingira kama vile kukata miti ovyo vinahatarisha maisha ya watu waishio vijijini.

**Mkakati:** Taarifa juu ya utunzaji mazingira ziandaliwe na kusambazwa kwa wadau wote kupitia mikakati mbalimbali. Vilevile mamlaka zinazoshughulika na mabadiliko ya tabia ya nchi zinapaswa kuwezeshwa ili kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**Mfano wa mkakati: kupunguza utegemezi wa kilimo cha mvua**

Mabadiliko ya tabia nchi huleta ukame na kuathiri sekta ya kilimo. Changamoto hii inaweza kushughulikiwa kwa kujenga miundombinu yenye kuwezesha kuvuna maji kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya maji na kuyahifadhi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

### Himiza maendeleo ya kilimo

**Hali halisi:** Wananchi waishio vijijini wanajishughulisha zaidi na kilimo na ndiyo kundi la watu masikini zaidi. Hii inaashiria kuwa tija katika sekta ya kilimo bado ipo chini. Utumiaji wa njia na zana duni za kilimo na ukosefu wa teknolojia ya kisasa na wataalamu wa kilimo ndizo changamoto kubwa zinazoikabili sekta hii.

**Mkakati:** Maamuzi katika sekta ya kilimo ni lazma yaongozwe na mipango ya muda mrefu ili kuleta tija. Mapinduzi yoyote ya kilimo ni vema yakatokana na utafiti wa kina. Ongezeko la maafisa kilimo wenye ujuzi wa kisasa na ushiriki wa sekta binafsi kwenye kilimo vitaongeza tija. Elimu ya kilimo ifundishwe pamoja na masomo ya ujasiriamali na masoko ili kuongeza ufanisi na ushindani katika sekta hii muhimu.

**Mfano wa mkakati: Uzalishaji mazao mseto**

Wakulima wanatakiwa kulima mazao mbalimbali ili kuifanya ardhi yao iendelee kuwa na rutuba na madini kwa muda mrefu. Hii itasaidia kukuza kilimo endelevu na itawaepusha na kuharibika kwa mazao lakini pia itawapatia uhakika wa kipato.

## 4.2 Utekelezaji – Hatua Sahihi za Kuchukua

Ili mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii uweze kutekelezwa kikamilifu nchini Tanzania inabidi, watu binafsi, mashirika pamoja na serikali wafundishwe na kuuelewa mfumo huu. Elimu ienezwe katika ngazi zote za jamii ili mfumo huu uweze kuwa wa watu wote. Makundi yafuatayo yatahusishwa katika utekelezaji wa mfumo huo.

## Serikali ya Tanzania

| | |
|---|---|
| **KWA NAMNA GANI** | Mfumo wenyewe pamoja na faida zake utawasilishwa serikalini na kuingizwa katika mipangilio ya maendeleo. |
| **KWA NINI** | Ili mfumo wa Uchumi Jamii uweze kutekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi, ni muhimu serikali kuutumia mfumo huu katika bajeti na mipango mbalimbali ya maendeleo. Hii itahakikisha kuwa kila Mtanzania ananufaika na matokeo chanya ya Uchumi wa Soko Jamii. |

## Sekta Binafsi na ya Umma

| | |
|---|---|
| **KWA NAMNA GANI** | Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii utafundishwa kwa wajasiriamali, wafanyabiashara ndogo ndogo, za kati na kubwa, na kwa mawakala wa uhusiano kibiashara na elimu. |
| **KWA NINI** | Hatua hii inahakikisha kuwa wadau wote wa sekta binafsi na sekta ya umma wanaelewa na kufahamu hatua na faida zinazotarajiwa kutoakana na mfumo huu wa kiuchumi na matokeo yake jambo litakalowafanya wajihusishe kwa hali na mali katika utekelezaji wa mfumo huu wa Uchumi wa Soko Jamii. |

## Wawakilishi wa Kisiasa

| | |
|---|---|
| **KWA NAMNA GANI** | Mafunzo yatolewe kwa wafanya maamuzi katika ngazi zote, kitaifa, kiwilaya na kwenye ngazi ya kata ili kuelimisha faida na tunu za mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. |
| **KWA NINI** | Kwa kuwahusisha wadau wanaohusika na kutoa maamuzi kunaleta uhakika wa kusambaa kwa taarifa hadi katika ngazi ya chini kabisa na ngazi ya juu ya serikali ambapo maamuzi yanaweza kuunda utaratibu mpya na sheria kurahisisha utekelezaji wa mfumo huu wa Uchumi wa Soko Jamii. |

## Jumuiya za Dini

| | |
|---|---|
| **KWA NAMNA GANI** | Viongozi wa dini watapata mafunzo kuhusu kanuni na tunu za mfumo wa Uchumi Jamii ili waweze kupeleka maarifa hayo katika taasisi zao. |

| | |
|---|---|
| **KWA NINI** | Dini ina nafasi kubwa sana katika maisha ya Watanzania wengi. Kwa hiyo viongozi wa dini wanaweza kubadilisha mitazamo na miundo ya taasisi zao, kwa sababu wanatenda kama walezi wa kimaadili na mienendo ya kitabia na wanamgusa kwa kiasi kikubwa mtu mmoja mmoja ambaye ni muumini wa taasisi zao. |


## Asasi za Kiraia na Mashirika

| | |
|---|---|
| **KWA NAMNA GANI** | Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii utafundishwa kwa asasi za kiraia ili uweze kueleweka na kuungwa mkono na asasi hizo, na hivyo kuzifanya zishiriki vizuri katika kuutekeleza mfumo huo. |
| **KWA NINI** | Hii itahakikisha kunakuwa na utekelezaji wa mfumo kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya juu, ikiongozwa na kanuni za ushirikiano na kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele vya watu na jamii iliyopo katika ngazi ya chini. Hapa uhuru wa mtu mmoja mmoja utazingatiwa katika ajenda ya ukuaji wa uchumi endelevu na shirikishi. |

## Watu wa Tanzania

| | |
|---|---|
| **KWA NAMNA GANI** | Hatua za utekelezaji katika sekta mbalimbali zitaenda sambamba na mafunzo kwa mtu mmoja mmoja katika ngazi za chini kabisa katika jamii. Baada ya hapo Watanzania wataarifiwa katika namna mbili: Kwanza watapata ujuzi kutoka kwa wadau wenye mafunzo wanaotoka kwenye makundi matano yaliyoelezwa hapo juu. Pili watapokea taarifa zaidi wakati wa mafunzo mahususi yatakayoandaliwa kwa ajili yao. |
| **KWA NINI** | Wananchi kwa kiasi kikubwa ndio wanufaika wakubwa wa mfumo wa Uchumi Jamii. Ili kunufaika na faida zilizoelezwa, ni lazima watu wawe na ufahamu na waelimishwe kuhusu kanuni na taratibu za mfumo wa Uchumi Jamii. Ni mpiga kura mwenye elimu sahihi tu ndiye anayeweza kufanya maamuzi sahihi juu ya wawakilishi wake na kutoa tathmini kuhusu ubora wa sera za nchi, kwa kujumuisha sauti za mtu mmoja mmoja, uhuru wao, juhudi binafsi, utu wa mtu na kuhakikisha haya yote yanaheshimiwa. |

**Kielelezo 9: Hatua za Utekelezaji**



# 5. Hitimisho

Serikali ya Tanzania imeandaa mipango muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu. Hata hivyo mafanikio katika utekelezaji wa mipango hii yanahitaji kila mwanajamii ashirikishwe na afaidike na maendeleo ya kiuchumi. Mfumo huu wa Uchumi wa Soko Jamii unaonekana kuwa chaguo sahihi kwa ajili ya uchumi imara, jumuishi na endelevu.

Mwenendo wa jumla wa maendeleo ya dunia umeonesha kuwa uchumi wa soko huleta mafanikio ya kiuchumi, uvumbuzi, na ubora wa bidhaa na huduma. Mapungufu ya uchumi wa soko huria yanatatuliwa na mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unatoa fursa ya kuibadilisha Tanzania kwenda kuwa nchi yenye uchumi imara na shirikishi.

Rais wa zamani wa Ghana, John Kufuor, alikubaliana na mtazamo kwamba Afrika inatakiwa kuuasili mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii: mtazamo ambao mwalimu Julius K. Nyerere alikuwa nao tayari na alipendekeza kwamba maendeleo ya kweli yapo ndani ya nguvu ya watu. Hii inapaswa kuwahimiza Watanzania kwamba sasa ni muda wa mabadiliko.

Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania unaangalia fursa katika sera za elimu na jamii ili kuhakikisha kwamba kila mwananchi anafaidika. Uwekezaji huu unawawezesha watu kujihudumia wao wenyewe na familia zao. Masikini na watu dhaifu hawatatengwa wala kuachwa nyuma. Kwa hiyo umakini unapaswa kuwepo ili kuboresha hali zao za maisha.

Ili kufikia hatua nzuri ya maendeleo kadiri iwezekanavyo, inashauriwa kwamba Tanzania ikubali kutumia mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kama mfumo mpya wa uchumi kwa ajili ya ukuaji shirikishi na endelevu wa uchumi kwa taifa na watu wake wote.

Muhtasari huu umetafsiriwa kutoka chapisho la kiingereza kuhusu Mfumo wa Soko Jamii nchini Tanzania. Wasomaji wa muhtasari huu wanashauriwa pia kusoma toleo la kwanza la kitabu kinachoelezea Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa mapana yake kwa ajili ya kupata uelewa zaidi.